# Nipashe

Jumatatu Julai 8, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579964

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Waziri Lugola ataka usafiri mabasi saa 24

UKURASA 2




UKURASA 13

# Msaidizi wa Membe adaiwa kutekwa Dar

**DADA** yake aeleza picha nzima ilivyokuwa, wengine wadaiwa kutekwa jimboni kwa Tundu Lissu... *Endelea uk. 2*



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na wa kutoka mikoa mbalimbali wakitembelea Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) katika Viwanja vya Julius Nyerere Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

## Spika Ndugai afunguka gharama matibabu yake

UKURASA 3

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**SABABU USITISHAJI WA SAFARI ZA TRENI**
SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limetangaza kusitisha baadhi ya safari zake za treni kutoka Dar es Salaam kwenda Isaka...

**UKURASA WA 21**

**WAGENI WANASWA MADAI YA KUTOROSHA DHAHABU**
LICHA ya serikali mkoani Mbeya kufungua masoko mawili ya kuuzia madini mkoani humo, imebainika...

## Hospitali maarufu hatarini kufungwa

UKURASA 3

**MICHEZO** STARS, AMUNIKE WAACHANA RASMI UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Lugola ataka mabasi kusafiri saa 24

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amepiga marufuku Makamanda wa Polisi wa Mikoa nchini kuyazuia mabasi yanayotoka mikoa ya Kanda ya Ziwa kwenda Dar es Salaam au kurudi Kanda ya Ziwa kusafiri muda wa usiku kwa kisingizio cha kuofia kuvamiwa na majambazi.

Lugola amesema Jeshi la Polisi lipo imara na kamwe haliwezi kucheka na majambazi wala kuwaonea huruma majambazi na kwanza kutupangia majambazi muda gani mabasi yasafiri na yasisafiri, mabasi hayo yanapaswa kusafiri saa 24.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara Kijiji cha Namibu Kata ya Neruma, Jimbo la Mwibara, wilayani Bunda, Lugola alisema mabasi yanayosafiri kutoka Kanda ya Ziwa kwenda Dar es Salaam yasizuiwe Morogoro na yanayotoka Dar es Salaam kwenda kanda ya Ziwa yasizuiwe Shinyanga kwa sababu zinazodaiwa za kiusalama.

"Mimi ndiyo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hatuwezi kupangiwa ratiba ya kusafiri na majambazi, Serikali ya Rais Magufuli ipo imara, na Polisi ipo imara, hivyo agizo hili ambalo pia niliwahi kulitoa lizingatiwe ipasavyo, niliagiza majambazi wote wasambaratishwe, asakwe mpaka jambazi wa mwisho, akamatwe kama kuku," alisema Lugola na kuongeza:

"Taarifa ya uhalifu inaonyesha Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa ya kupambana na uhalifu na hasa uhalifu wa majambazi, na niliwahi kuagiza kipindi hiki si cha kuwa na huruma na majambazi ni kipindi cha kuwashughulikia ili wananchi waishi kwa amani."

Lugola alifafanua kuwa, nchi haiwezi kupangiwa na majambazi muda wa kusafiri, kufanya biashara, hivyo maelekezo aliyoyatoa kwa Jeshi la Polisi liendelee kupambana na majambazi popote walipo nchini.

"Nimeelekeza magari yanayosafiri yasizuiwe Morogoro yanapopita muda wa usiku saa nne usiku na kuendelea, yasizuiwe Shinyanga, ili majambazi wajue popote walipo wapo imara wamejipanga vizuri na mimi waziri wao nipo imara kuhakikisha Jeshi la Polisi linawashughulikia majambazi mmoja baada ya mwingine ili kuwafanya wananchi katika nchi yao waendelee kushughulika na masuala ya kujijengea uchumi ili Serikali ya Rais Magufuli, iweze kuwa na uchumi wa kati na majambazi wote wakamatwe kama kuku," alisema Lugola.

# Msaidizi wa Membe adaiwa kutekwa

**Na Mwandishi Wetu**

MSAIDIZI wa Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, Allan Kiluvya, anadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana maeneo ya Mbezi Jogoo, jijini Dar es Salaam.

Mtoa taarifa ambaye amejitaja kwa jina moja la Magreth mkazi wa Jogoo, amejirekodi kupitia mtandao wa kijamii akieleza Allan alivyotekwa na kisha sauti hiyo kuitupia mtandaoni.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alipopigiwa simu kuhusiana na tukio hilo, alisema hana taarifa kama kuna mtu ametekwa.

"Sina taarifa kama kuna mtu ametekwa, lakini kama mtu ametekwa si unaliarifu Jeshi la Polisi ili wafanye uchunguzi, unatuma mitandaoni, ndiyo maana tunatilia shaka," alisema.

Awali, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Mussa Taibu, alisema tukio hilo ni jipya kwake.

"Ninashangaa sijui kuna wimbi gani, huyu shetani sijui anatoka wapi? Nitafuatilia kama kuna ukweli wowote ila kwangu bado halijanifikia," alisema Kamanda Taibu.

Katika maelezo yake Magreth aliyojirekodi kuhusiana na tukio hilo, alidai kuwa alikuwa yeye na dada yake Agnes pamoja na Allan, katika hoteli ya Juliana iliyoko Mbezi Africana.

"Nilikuwa mimi, Allan na dada yangu mwingine anaitwa Agnes. Tulikuwa hoteli ya Juliana kule Africana, baada ya kunywa ulifika muda wa kwenda nyumbani, Allan akasema atatupeleka, si mbali na hapo Juliana, ni Jogoo kituo kinachofuata. Alitupeleka hadi nyumbani, nikashuka na kufungua geti akaingiza gari akashuka Allan na dada yangu.

"Allan alitaka kumsalimia mama yake ambaye wakati huo alikuwa hajalala. Alimsalimia wakaongea muda wa kuondoka aliniambia nimfungulie geiti ili atoke. Nilifungua na kulifunga, nilikuwa nimemwomba fedha, si unajua ile kikaka kaka aniachie 'pocket money' (fedha za matumizi) kidogo, akaniambia niende nje tuongee. Akarudi kinyume nyume, nikafunga geti, nikatoka nje. Nilipotoka nikasogelea gari lake kwa mbele ambako Allan alikuwa anaelekea kulikuwa na gari lililokuwa likipandisha kwa sababu kuna kibonde, ilikuwa inaelekea upande wa kulia alikokuwa Allan," alisema.

Magreth aliendelea kusimulia

INAENDELEA UK. 8



Wakazi wa Mji Mdogo wa Ilula wilayani Kilolo mkoani Iringa, wakichota maji baada ya kukamilika kwa mradi wa maji hivi karibuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# ...Chadema yadai viongozi kwa Tundu Lissu kutekwa

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimedai, kutekwa na kuteswa kwa viongozi na baadhi ya wanachama wa chama hicho Jimbo la Singida Mashariki.

Chama hicho kimedai kuwa kitendo hicho kimefanywa na vijana wa ulinzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) cha Green Guard katika jimbo hilo.

Katibu wa Chadema Kanda ya Kati, Idd Kizota, amedai viongozi hao walikuwa katika ofisi za chama hicho katika jimbo hilo katika kikao cha ndani kwa lengo la kufanya uchaguzi mbalimbali wa chama, na baadaye kuvamiwa na vijana hao na viongozi wao wawili kutekwa na kupelekwa kusikojulikana.

"Pia walivunja kioo cha gari letu moja aina ya Ford Ranger ingawa dereva alifanikiwa kuwakimbia," Kizota alisema.

Viongozi wanaodaiwa kutekwa na kuteswa ni Mwenyekiti wa Chadema Jimbo la Singida Mashariki, Agnesta Lambat na Diwani wa Kata ya Misughaa, Jumanne Rajab.

Alisema kwa Agnesta yupo hospitali ya Benjamin Mkapa akipatiwa matibabu, huku diwani akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Nakiungu mkoani Singida.

"Agnesta alikuwa na hali mbaya zaidi, tulimpeleka Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma, lakini Rajab Jumanne yeye tulimpeleka katika Hospitali ya Makiyungu Ukungi," Kizota alisema.

**KAULI YA JESHI LA POLISI**

Akizungumzia madai hayo ya viongozi wa Chadema, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Switbeth Ngiwike, alisema anashangaa madai hayo ya watu kutekwa na kuahidi kuwa Jeshi la Polisi litatoa taarifa kuhusiana na suala hilo leo.

"Hii lugha ya kutekwa, kuteswa sijui inatoka wapi, tutatoa taarifa kesho kuhusiana na hilo," Kamanda Ngiwike alisema.

Wiki iliyopita Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, alitangaza ratiba ya kufanyika kwa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Singida Mashariki Julai 31, mwaka huu.

Jaji Kaijage alisema fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa kati ya Julai 13 na 18, mwaka huu na uteuzi wa wagombea utafanyika Julai 18, alisema kampeni za uchaguzi zitafanyika kuanzia Julai 19 hadi 30.

Uchaguzi huo unafanyika kujaza nafasi ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Tundu Lissu, ambaye amevuliwa nafasi hiyo na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa maelezo kuwa amepoteza sifa.

## HABARI KITAIFA

# Ndugai afunguka gharama matibabu yake

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema anashangazwa na taarifa kuhusu gharama za matibabu yake alizotumia nchini India, zilizotolewa mwishoni mwa wiki na Baraza la Wazee la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Ijumaa iliyopita, viongozi wa baraza hilo la wazee, walizungumza na vyombo vya habari huku wakitaka ripoti ya gharama za matibabu ya kiongozi huyo wa chombo cha kutunga sheria, iwasilishwe bungeni kutokana na gharama zilizodaiwa kuwa ni kubwa.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hashim Issa, alisema jijini Dar es Salaam katika mkutano huo na waandishi wa habari kuwa ndani ya matibabu hayo kuna harufu ya ufisadi.

Issa alidai kuwa matibabu ya Spika Ndugai yalitumia Dola za Kimarekani milioni 12 na kwamba huo ni ufisadi uliolenga kuvusha fedha ambazo ni kodi za Watanzania.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kutoka Kongwa mkoani Dodoma, Ndugai alisema ameshtushwa na taarifa hizo ambazo alisema zina lengo la kumchafua kisiasa.

"Kwanza ni lazima mtu ajue hizo dola ni sawa na shilingi ngapi za Kitanzania. Hivi kuna ukweli wowote kuhusu gharama hizo? Na wamezipata wapi? Kama ni kweli wajiulize kwa mwezi nilikuwa natumia Dola ngapi na kwa wiki kiasi gani na kwa siku hivyo hivyo.

"Naomba niweke wazi kwamba takwimu hizo ni za kupikwa na kwa nini wahoji sasa gharama hizo na kudai ni kubwa? Gharama nilizotumia ni ndogo sana ukilinganisha na zile za Ulaya kama Ubelgiji anakotibiwa Tundu Lissu," alisema.

Ndugai pia alisema kwa kiasi hicho cha fedha kilichodaiwa kutumika, ni lazima mtu ajiulize ni dawa kiasi gani alitumia na matibabu husika yalihusu nini hadi kufikia kiasi hicho.

Sambamba na hilo, alisema matibabu ya viongozi na watumishi wa serikali nchini India yanafanyika katika hospitali za gharama nafuu ambazo zimeingia mkataba na serikali. Pia alisema matibabu hayo hufanyika bila kutanguliza malipo na serikali hulipa baada ya kupatiwa ankara za madai.

"Wanaosema kuwa nimetumia dola milioni 12 na kwamba kuna harufu ya ufisadi nawashangaa sana. Kama nilivyosema gharama hizi ni kwa mkataba na zinalipwa baadaye, sijui kama serikali imeshalipa. Ni vyema wakajiridhisha na kauli zao kabla ya kuwachafua watu," alisema.

**WALIVYOSEMA WAZEE CHADEMA**

Issa alisema: "Tunataka kuona ripoti zote zinawasilishwa bungeni, vikiwamo vyeti vya matibabu na madaktari walifanya operesheni," alisema na kudai kuwa Spika Ndugai alikwenda nchini India kutibiwa ingawa hawajui alikuwa anasumbuliwa na nini.

"Matokeo yake alivyorudi Tanzania akasema ametumia Dola za kimarekani milioni 12. Maradhi gani hayo? Kafanya operesheni ngapi? Alikwenda hospitali ya aina gani mpaka alipe dola milioni 12. Hakuna duniani, huo ni ufisadi.

"Hiyo ilikuwa njia ya kuvusha fedha ambazo ni kodi za Watanzania kutumia kisingizio cha maradhi kwenda hospitali, kumbe kavusha fedha," alidai huku akisisitiza Baraza la Wazee Chadema, linataka kuona ripoti zote zinawasilishwa bungeni.

"Ripoti ya Spika Ndugai, tunataka vyeti vyote vya hospitali, hesabu ya madaktari, alifanyiwa operesheni ngapi. Tunataka hesabu kamili ya miezi yote ya matibabu kama zimefika Dola za kimarekani milioni 12," alisema.

Hata hivyo, Aprili 14, mwaka huu, Spika Ndugai akijibu swali la gharama ya matibabu yake nje ya nchi wakati akizungumza na waandishi wa habari, hawezi kujua kama kuugua kwake kumelisababishia taifa fedha nyingi.

"Labda ningekufa watu wangefurahi. Katika matibabu yoyote yale, tunawatibu watu hatuangalii thamani ya mtu na kiwango cha fedha kilichotumika. Kinachoangaliwa kama kuna matumizi mabaya ndani ya matumizi hayo," alisema.

"Nilitibiwa mwaka 2015/16 na hesabu hizo ni za 2017/18. Unajua tena mtu akibanwa anatafuta sababu huku na kule. Wanaotibiwa ni wengi na hospitali niliyokwenda kutibiwa ni ya kawaida. Nilikutana na Watanzania wa kila aina, wa aina zote, tunapishana huyu anakwenda kwa daktari huyu, mwingine huyu, sijawahi kwenda hospitali ya New York (Marekani), Ujerumani, naenda India ambako ndiko Watanzania wanakotibiwa," aliongeza.

# Hospitali maarufu hatihati kufungwa

**Na George Tarimo,** MAKETE

UONGOZI wa Shirika la Consolata Fathers, linalomiliki Hospitali ya Ikonda, Makete mkoani Njombe, umetishia kuifunga hospitali hiyo kwa madai ya kuwapo urasimu unaofanywa na baadhi ya taasisi za serikali.

Kwa mujibu wa uongozi huo, changamoto kubwa zinazotishia kufungwa kwa hospitali hiyo, ni kutoridhishwa na urasimu wanaofanyiwa ikiwamo vifaa tiba wanavyoagiza kutoka nje ya nchi, kucheleweshwa kuwafikia kwa wakati.

Mtawala wa Hospitali hiyo, Padri Alessandro Nava, alisema juzi kuwa jambo hilo na mengine ambayo yanachangiwa na baadhi ya taasisi za serikali na kwamba baadhi ya watumishi wanaweza kuondoka nchini iwapo hazitatuliwa.

Padri Nava pia alisema kumekuwa na madai kwamba anaigombanisha hospitali hiyo na serikali jambo ambalo alisema si kweli.

"Wakati wa Pasaka, nilitaka kufunga hospitali hii kwa sababu kadiri tunavyoendelea kusaidia watu, wao wanaendelea kutuangamiza tena wameonyesha kwenye vyombo vya habari hospitali hii na kusema mimi ninagonganisha watu dhidi ya serikali. Kama ni hivyo basi tufunge tuondoke zetu japo mimi sikuja Tanzania kugonganisha watu bali nilikuja kusaidia," alisema.

"Nimekutana mara mbili na Rais (wa awamu ya kwanza Julius) Nyerere mwaka 1999 Nairobi nchini Kenya. Walikusanyika wakuu wa ushirika kutoka duniani kote kujadili hospitali, karakana na shule mbalimbali ziendelee au tuache. Nyerere alisema ninyi endeleeni kama mlivyokuwa mkifanya zamani."

Padri Nava aliitaja pia barua ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe aliyowaandikia Machi 20, mwaka huu, yenye malalamiko na maonyo mengi lakini akasema hospitali wamejibu vizuri na kurudisha majibu kwake na kuinakili kwenye ofisi mbalimbali ikiwamo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Pia alisema aliomba kukutana na Rais John Magufuli ili kumweleza changamoto hizo na kwamba akipata nafasi hiyo atamweleza yaliyo moyoni mwake.

"Nitamweleza kwa uwazi kwamba Mheshimiwa Rais wewe unajitahidi, nimeona ukisaidia maskini na umesema maskini lazima tuwasaidie. Sisi tunataka kukusaidia katika lengo hili lakini mbona wanatuzuia na kuhoji tusiwasaidie?

"Sasa kama ni kweli yeye atuambiye tuendelee au tusiendelee kwa sababu sisi kuacha hatukufika Tanzania kufanya biashara na tunataka kuweka vifaa vya kisasa ambavyo tunaagiza kutoka Ulaya lakini tunaogopa kwa sababu tunavyoendelea kuboresha hospitali tunapata vikwazo vingi," alisema Padre Nava.

Alisema wanataka kuweka mashine za kisasa na kwamba mashine hizo ziko Ulaya zinakuja muda mrefu, lakini wanaogopa kwa

INAENDELEA UK. 8


LAS VEGAS CASINO

EMPLOYMENT OPPORTUNIES

1 EXPERIENCED-DEALERS
2 TRAINEE DEALER
3 CASHIERS
4 ATTENDANTS
5 WAITRESSES
6 BAR SUPERVISOR
7 SECURITY

We are looking for suitable Applicants to fill the above positions. Applicant should indicate the position interested.

**Qualifications:** Applicants should be educated of not less than Form IV and above, with good knowledge of English and Mathematical calculations.

**Minimum age 20 years old.**

***Attractive salaries and benefits await those to be selected.***

***All suitable applicants will be contacted for a formal interview.***

**General Requirements:**

**Application should be accompanied by:**

- Detailed C.V.
- Copies of relevant certificates: Academic and Work related (if any)
- 2 passport size coloured photographs
- 2 names of referees and their tel. numbers
- Applicant's Day-time telephone number.

Letter of Application should be addressed to Casino Manager and handed to reception desk from 9:am to 4:pm, at Las Vegas Casino, Ali Hassan Mwinyi Road, Upanga, not later than **30/07/2019.**

115311602

# Waziri atishia kumsweka ndani mkandarasi maji

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ametishia kumweka ndani kwa siku tano mkandarasi Geofrey Oyao kutoka Kampuni ya Orientation Construction Ltd. anayetekeleza mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria katika miji wa Isaka na Kagongwa.

Mbarawa alitoa kauli hiyo jana alipotembelea eneo la mradi la Kagogwa na Isaka kwenye utandazaji wa mabomba.

Profesa Mbarawa amefikia hatua hiyo kutokana na kusuasua kwa mradi huo huku mkandarasi huyo akitoa ahadi za uongo hali iliyosababisha mradi kushindwa kukamilika.

Alimpatia mkandarasi mwezi mmoja ili kukamilisha kwa kuandikishana kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya mbele ya kamati ya ulinzi na usalama na kuweka ahadi ya kukamilisha mradi huo kwa maandishi.

Ilidaiwa kuwa mradi ulipangwa

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA), wajumbe wa Bodi ya Maji, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mabanda ya Rita, Maliasili, Nida yavuta wengi Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

WAKAZI wa Jiji la Dar es Salaam jana walifurika kwa wingi katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salam (DTIF), Banda la Maliasili na Utalii, Nida na Rita yakionekana kufurika zaidi.

Japokuwa mabanda yaliyoshiriki katika maonyesho hayo mengi yake yalikuwa na watu wengi, lakini mabanda hayo matatu yalifurika zaidi.

Kila mmoja aliyefika katika mabanda hayo alionekana kupambana na msukumano kwa kuhakikisha anapata huduma.

Katika Banda la Nida, wananchi waliohojiwa walisema wanafuata huduma ya vitambulisho vya taifa.

Aidha, la Rita pia, wengi walisema wanafuata vyeti vya kuzaliwa vyao na vya watoto.

Katika Banda la Maliasili na Utalii, wengi walisema wanakwenda kuangalia wanyama.

Katika Banda hilo la Maliasili na Utalii, mbali na kuangalia wanyama, pia wengi wao walifurika kuangalia kijiji cha mfano katika banda la Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kilichohifadhi mazingira kando kando ya safu za milima ya maporomoko ya maji.

Pia banda hilo ndilo lililoonekana kuwa na idadi kubwa ya watoto na Nipashe lilipowahoji, walisema wanapendelea kwenda zaidi katika banda hilo kwa sababu ya kuangalia wanyama.

"Nilikuwa nasimuliwa tu kwamba Sabasaba kuna wanyama pia, na ndio maana nikaja kujionea na nimeona wanyama wengi," alisema mmoja wa waliofika katika banda hilo la Maliasili ya Utalii, Lucy Moses.

Akizungumzia maonyesho hayo, Naibu Waziri wa Viwanda na biashara, Stella Manyanya, alisema wananchi wameanza kuelewa maonyesho hayo.

Alisema ni vema wanaokwenda kujionea na kujifunza mambo mbalimbali katika maonyesho hayo, ana kwenda kufanya kwa vitendo shughuli za kujiingizia kipato kwa kasi zaidi.






# Sababu usitishaji wa safari za treni

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limetangaza kusitisha baadhi ya safari zake za treni kutoka Dar es Salaam kwenda Isaka, Kahama kwa saa 72 sawa na siku tatu kwa wiki kwa ajili ya matengenezo kwa miezi mitatu mfululizo.

Pia limesema kusitishwa kwa safari hizo, TRC itapoteza kiasi cha fedha Sh. bilioni 1.8 ya mapato yake ambazo zilikuwa zikiingizwa wakati treni hiyo ikifanya safari zake.

Akizungumza na waandishi wa habari katika banda la shirika hilo katika Maonyesho ya Biashara ya 43 ya Kimataifa Sabasaba, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema njia hiyo itafungwa kila siku ya Ijumaa hadi Jumapili kwa miezi mitatu mfululizo hadi mitano.

Alisema usitishwaji huo utajumuisha baadhi ya madaraja na makaravati kujengwa upya, kukarabati reli za zamani pamoja na kuimarisha reli toka Dar es Salaam hadi Isaka kwa umbali wa kilometa 970.

"TRC inapita katika mabadiliko makubwa kwa sababu serikali imeweka nguvu kubwa huko na kukamilika kwa kazi hiyo kutasaidia njia ya reli ipitishe treni kwa usalama zaidi, kuboresha zaidi huduma zake," alisema Kadogosa.

Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema treni zilizokuwa zikifanya safari Kamata hadi Pugu na Kamata kwenda Ubungo zitaendelea na ratiba ya siku tano tu kwa wiki.

Akitangaza ratiba ya safari ya treni hizo, Kadogosa alisema treni za kawaida za safari za Dar es Salaam-Kigoma-Mwanza na Mpanda, treni zitakuwapo kila Jumatatu hadi Jumatano.

Safari za Kigoma kwenda Dar es Salaam zitakuwa kwa siku mbili pamoja na ile ya Mwanza kwenda Dar es Salaam.

Kwa upande wa treni za Deluxe kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, alisema itakuwapo siku moja huku Kigoma hadi Dar es Salaam itakuwa siku moja pia.

Alisema uboreshwaji wa njia hizo ulianza rasmi jana.

# HABARI KITAIFA



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, (wa pili kushoto), akimsalimia mkazi wa Kijiji cha Namibu, Kata ya Neruma, Jimbo la Mwibara, wilayani Bunda Mkoa wa Mara jana, alipofanya ziara. Habari Uk. 2. **PICHA: WMN**

## Polisi waua mtuhumiwa wa ujambazi sugu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limemuua kwa kumpiga risasi mtuhumiwa sugu wa ujambazi ambaye alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu kutokana na kujihusisha na matukio ya kihalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alitoa taarifa hiyo jana wakati alipozungumza na wananchi wa Mtaa wa Umbembeni wilayani Kondoa mahali alipouawa mtuhumiwa huyo.

Muroto alitaja jina la aliyeuawa ni Sostenes Muganyizi maarufu 'Rasta' ambaye alikuwa akitafutwa na Jeshi la Polisi kutokana na kudaiwa kujihusisha na vitendo vya kihalifu katika maeneo mbalimbali nchini.

"Mtu huyu tumekuwa tukimtafuta kwa muda mrefu na amekuwa akijihusisha na matukio ya ujambazi katika maeneo mbalimbali nchini," alisema.

Alisema jambazi huyo aliuawa baada ya kujaribu kurushiana risasi na askari polisi katika mtaa wa Umbembeni wilayani Kondoa, ambapo alikuwa anajaribu kuwatoroka baada ya kutaka kukamatwa.

Kamanda Muroto alisema tukio hilo lilotokea majira ya asubuhi ambapo mtu huyo alikuwa amejificha katika moja ya nyumba ya mkazi wa Wilaya ya Kondoa ndipo Jeshi la Polisi lilipofanya uchunguzi na kumbaini.

Akielezea zaidi, Kamanda Muroto alisema mtu huyo alikuwa akijaribu kuwakimbia, huku akijihami kwa akipiga risasi tatu zilizowakosa askari polisi waliotaka kumkamata.

Alisema kutokana na mafunzo walinayo askari hao, walifanikiwa kumuua akiwa katika harakati hizo za kuwakimbia.

Muroto alisema na kwa sasa Jeshi la Polisi linamshikilia mmiliki wa nyumba ambayo mtuhumiwa huyo alikuwa amejificha, ingawa hakutaka kumtaja jina.

Kamanda huyo aliwataka wananchi mkoani hapa kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo katika kupambana na uhalifu.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Umbembeni Mjini Kondoa, Hussein Dabo, alilishukuru jeshi hilo kwa kazi nzuri wanayofanya.

Dabo alisema kumekuwa na matukio mengi ya wananchi kuibiwa na wengine kunyang'anywa mali zao na watu wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu.

Alisema wataendelea kutoa taarifa za wahalifu katika maeneo yao ili kudhibiti vitendo hivyo.

## Wodi ya watoto yazidiwa wagonjwa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Sumbawanga mkoani Rukwa, imeelemewa na wagonjwa katika wodi ya watoto, hali inayosababisha kuwalaza zaidi ya mmoja katika kitanda kutokana na kuwa na eneo dogo la kuwalaza wagonjwa hao.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Kelly Msafiri, alisema hali hiyo inatokana na wodi hiyo kuwa na eneo dogo ambalo linachukua vitanda 12 tu.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo inapokea watoto wanaopewa rufani kutoka katika maeneo mbalimbali mkoani humo, hivyo kuwa na wagonjwa wengi hali inayosababisha kukosa eneo la kuwalaza na matokeo yake wamekuwa wakiwalaza zaidi ya mgonjwa mmoja katika kila kitanda.

Mganga huyo alisema hali hiyo ni tishio kwa afya zao kwani wanaweza kuambukizana magonjwa, hivyo kuiomba serikali na wadau wengine kuwasaidia kujenga wodi nyingine ambayo itakuwa na eneo la kutosha.

Alisema hospitali hiyo ina hadhi ya rufani, hivyo ni vizuri ikawa na miundombinu inayoendana na hadhi yake ili kukidhi mahitaji kwa kuwa kupandishwa hadhi kwa hospitali hiyo kumesababisha ongezeko la wagonjwa.

Naye Mwajuma Salleh, mama wa mmoja wa watoto waliolazwa katika wodi hiyo, alisema hali hiyo inatisha na inakatisha tamaa kwa kuwa wanaingiwa na hofu ya watoto wao kuugua magonjwa mengine kutokana na kulala zaidi ya mmoja katika kitanda kimoja.

"Tunaomba serikali iliangalie hili, tunashukuru hivi sasa huduma zimekuwa bora, lakini zipo baadhi ya changamoto ambazo inapaswa kufanyiwa kazi ili iendane na maboresho hayo kwani kitendo cha kulaza wagonjwa zaidi ya mmoja katika kitanda kimoja ni hatari, inaweza kusababisha hata baadhi ya wagonjwa kuanza kuikimbia hospitali hii," alisema.

## Takukuru yabaini madudu mil. 220/- ukarabati hospitali

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Lindi, imeanza kufuatilia matumizi ya Sh. 221,000,000 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya majengo katika Hospitali ya Mkoa huo Sokoine.

Mkuu wa Taasisi hiyo, Stephen Chami, ameyaeleza hayo alipokuwa anaelezea utekelezaji uliofanywa katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Chami alisema serikali iliupatia Mkoa wa Lindi kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya marekebisho ya wodi ya watoto, choo cha wagonjwa na matangi mawili yenye ujazo tofauti jumla ya lita 200,000.

Chami alisema Dawati la Utafiti na Udhibiti lilipofuatilia, limebaini fedha za ukarabati zimeisha wakati ukarabati ukiwa haujakamilika, huku baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya kazi husika kutoonekana, na hakuna maelezo yoyote juu ya upotevu wake.

Kutokana na mapungufu hayo, Chami alisema Takukuru Mkoa imeanza kuchunguza kwa kina ili kubaini waliohujumu ukarabati huo na wale watakaobainika watafikishwa mahakamani.

"Hivi sasa tunaendelea na uchunguzi wetu, ikiwa ni pamoja na kukusanya vielelezo ili tujiridhishe na hiyo hali, na pale tutapogundua madudu tutachukua hatua mara moja," alisema Chami.

Aidha, alisema katika kipindi cha Aprili mosi hadi Juni 30, mwaka huu, taasisi hiyo ilifuatilia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Rutamba, Mnara hadi Nyengedi yenye urefu wa kilomita moja inayojengwa na Kampuni ya Nyumbani Construction Limited na kubaini mapungufu mbalimbali.

Chami alisema barabara hiyo inayojengwa kwa gharama ya Sh. 302,018,900, wamebaini maeneo ya makaravati kuwa na nyufa kabla ya kuanza kutumika, na kumtaka mkandarasi kufanya marekebisho kwa kasoro zilizobainika kabla hajafikia mwisho.


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

**NOTISI/ TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na FIRST NATIONA BANK (FNB), MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | STEPHEN BUDEBA NDAKI | STEPHEN BUDEBA NDAKI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 58602 LR MWANZA L.O. NO.620707, KIWANJA NO. 293, BLOCK A, NYAMHONGOLO – ILEMELA MWANZA | 23/07/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | ANTHONY NESTORY MDULA | ANTHONY NESTORY MDULA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 41609 LR MWANZA KIWANJA NO. 904, L.O. NO. 403104, BLOCK A, BUSWELU KASIKAZINI - MWANZA | 23/07/2019 SAA 08:00 MCHANA |

**Masharti ya mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NASI KUPITIA ANUANI HIZI:**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**MASETO AUCTIONEER,**
**P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM**
**+255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU +255 762 260 787**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili Bara uendane na maandalizi U-20

**BAADA** ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kufungua rasmi dirisha la usajili, klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili zimekuwa zikitangaza wachezaji wake wapya iliyowasajili.

Timu zote zimekuwa zikijipanga kusajili wachezaji wapya, kwa sababu ya lengo moja kuu la kuimarisha vikosi vyao, kuelekea msimu mpya wa mwaka 2019/20, ambao utaanza baadaye mwezi ujao.

Lengo la kusajili wachezaji wapya linaashiria kila timu inahitaji kutwaa ubingwa katika mashindano itakayoshiriki, au kumaliza kwenye nafasi za juu tatu katika msimamo wa ligi husika.

Inaaminika kuwa, wachezaji wapya wanaosajiliwa, wanaingia kikosini kwa ajili ya kuongeza nguvu kazi na si kuifanya klabu ipate matokeo mabaya.

Hakuna klabu inayosajili wachezaji wapya, huku ikitegemea kufanya vibaya katika ligi au mashindano yoyote ambayo itaalikwa au itashiriki kulingana na kanuni na taratibu za michuano hiyo.

Lakini ili klabu hizo ziweze kufanya vema katika mashindano ya hapa nchini, au ya kimataifa, ni lazima pia zikumbuke kuandaa wachezaji chipukizi.

Nipashe linazikumbusha klabu zote za hapa nchini, hasa zile zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kuhakikisha pia zinasajili wachezaji wenye vipaji kwa ajili ya kuzitumikia timu hizo katika vikosi vyao vya umri chini ya miaka 20.

Timu zitakapoandaa wachezaji wazuri katika timu zake za vijana, zitajiweka katika mazingira mazuri ya kutumia kiasi kidogo cha fedha katika kipindi cha usajili kwa kuwapandisha wachezaji wake waliofanya vema.

Kwa mfano sasa, Simba inajivunia kiungo wake, Jonas Mkude, kutoka Simba B wakati Yanga yenyewe ina wachezaji nyota kadhaa akiwamo beki, Paul Godfrey ambao wamekuwa na mchango mkubwa na wakipata namba katika kikosi cha kwanza cha timu hizo.

Kama klabu zitaishia kuweka ngumu katika timu za wakubwa, hii inamaana kuwa vikosi vyao vya pili vitaendelea kuwa ni timu za "zima moto", yaani timu zinazokuwapo kwa ajili ya kukidhi taratibu na kanuni za TFF.

Umefika wakati, klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, zikabadilika kwa kukubali kuandaa wachezaji wao, ambao asilimia kubwa ndio huja kuitumikia Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Kufanya vema kwa timu za vijana au kuwapo kwa ligi bora ya vijana ya U-20, ndio njia pekee ambayo itaifanya Taifa Stars kuimarika kwa sababu kwa sasa bado Tanzania haina wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa katika nchi za Ulaya kama ilivyo kwa majirani zetu Kenya (Harambee Stars) na Uganda (The Cranes), ambao wameambulia pointi katika mechi zao za hatua ya makundi kwenye Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019). Stars iliondolewa katika fainali hizo ambazo zinatarajia kuingia katika hatua ya robo fainali bila ya kupata pointi hata moja, wakati Uganda iliyofika hatua ya 16 Bora ilimaliza Kundi A ikiwa katika nafasi ya pili kwa kujikusanyia pointi nne, huku Harambee Stars wakitoka na pointi tatu.

Nipashe linaamini kuwa moja ya njia ya Taifa Stars kupata mafanikio, ni kwa klabu za Tanzania kuwaandaa vema wachezaji wake vijana ambao baadaye huitwa katika kikosi hicho na kupeperusha bendera ya nchi wakiwa ni wenye kujiamini na wenye uwezo wa kupambana.

Tunaamini kuwa katika mpira hakuna njia ya mkato au miujiza, maandalizi sahihi, ndiyo yanayoweza kuipa nchi mafanikio na si jambo lingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Viongozi wanapopuuza kubadili kanuni za ligi

Na Adam Fungamwango

**WIKI** iliyopita kwenye safu hii niliandika makala yenye kichwa cha habari 'Viongozi wajipange kubadilisha kanuni Ligi Kuu'.

Makala hiyo ilikuwa ikiwahamasisha viongozi wa klabu kupeleka mapendekezo ya kanuni mpya za Ligi Kuu msimu ujao wa 2019/20.

Niliandika kushangazwa na baadhi ya viongozi wa klabu mbalimbali kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu iliomalizika kulalamikia baadhi ya kanuni za ligi.

Mfano kuna kanuni ya mapato ya mlangoni ambapo timu mwenyeji inachukua mapato yote.

Nilikuwa nikishangaa baadhi ya viongozi wakipinga hilo wakati ni kanuni iliyopitishwa na wao wenyewe.

Lakini sababu kubwa ilikuwa ni kwamba viongozi wengi wa ligi wao wako bize kwenye kusajili wachezaji na mambo mengine ya klabu na kusahau kabisa kupeleka mapendekezo, au marekebisho ili Shirikisho la Soka Nchini (TFF) iyapeleke kwenye Kamati ya Utendaji na mwisho wa siku kupigiwa kura ya kupitishwa au la.

Wengi hawajishughulishi na hilo na wanakuja kuzishtukia zikiwa zinatumika, wanaanza kushangaa.

Hali hiyo imejitokeza tena kwenda kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu. TFF tayari imepokea mapendekezo, lakini taarifa zinasema kuwa mwitikio wa viongozi wa klabu mbalimbali za ligi kuu umekuwa mdogo. Ina maana yale yale yaliyotokea kwa msimu uliopita yamejitokeza tena.

Ni viongozi wachache sana waliojitokeza kupeleka mapendekezo ambayo yatakwenda kuwa kanuni msimu ujao. Nilitegemea kutokana na viongozi wengi kuonekana kukerwa na suala ya mapato kuchukua mwenyeji, basi wangejitokeza kwa wingi kupeleka mapendekezo mengine kuwa msimu ujao klabu zigawane mapato nusu kwa nusu, lakini wapi.

> **Ni viongozi wachache sana waliojitokeza kupeleka mapendekezo ambayo yatakwenda kuwa kanuni msimu ujao. Nilitegemea kutokana na viongozi wengi kuonekana kukerwa na suala ya mapato kuchukua mwenyeji, basi wangejitokeza kwa wingi kupeleka mapendekezo mengine kuwa msimu ujao klabu zigawane mapato nusu kwa nusu, lakini wapi.**

Kelele zote zile, lakini hakuna aliyekwenda kupeleka mapendekezo ili yapelekwe kwenye kamati, ngoja sasa ligi ianze ndiyo utaanza kuona shutuma na malalamiko.

Ina maana wadau wachache waliojitokeza, kama hakuna aliyependekeza hilo, basi msimu ujao tunaweza kuona robo tatu ya kanuni kama si zote ni zile zile tu za Ligi Kuu msimu uliopita.

Suala lingine ambalo wengi walilipigia kilele ni juu ya klabu za Ligi Kuu kucheza mechi za 'play off' dhidi ya timu za Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Baada ya Mwadui na Kagera Sugar kufanikiwa kurejea Ligi Kuu dhidi ya Pamba na Geita FC, wadau wengi walionekana kusikitishwa na hilo.

Wengi wakataka timu za Ligi Kuu zitakazokamata nafasi ya 17 na 18 zisicheze 'play off' na timu za Daraja la Kwanza, badala yake zicheze zenyewe kwa zenyewe na timu za Daraja la Kwanza zicheze zenyewe kwa zenyewe.

Wakapendekezwa iwekwe kwenye kanuni ya msimu ujao. Na hili lilionekana kuungwa mkono hata na mashabiki wengi mitaani ambao walitaka Mwadui ingecheza na Kagera Sugar na Pamba ingecheza na Geita FC. Kutokana na taarifa kuwa viongozi wengi wa klabu wameonekana kukacha kupeleka mapendekezo, sidhani kama haya yote ambayo wadau wanayataka yatakuwapo. Kama yanakuwapo basi itakuwa ni bahati tu. Kingine inawezekana kabisa serikali ambayo nayo ni mdau wa soka, ikapeleka TFF mapendekezo ya kutaka wachezaji wa kigeni wawe watano tu ndani ya uwanja kama vile Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe alivyotaka.

Sasa kama hakutokuwa na kiongozi wa klabu yoyote hasa wa Simba au Yanga kwenda kutetea au kutaka wachezaji wote 10 wa kigeni wacheze, basi inawezekana kanuni ya wachezaji watano tu wa kigeni kuruhusiwa kucheza ikapitishwa na kuanza kuzua mtafaruku na manung'uniko.

## MJADALA/BARUA

## Nakereka na tabia ya aina hii!

**Mhariri**

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani. Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili. Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimweleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake. Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

*Ni muhimu watu hao wakaelewa kwamba ndani ya usafiri wa umma, kila mtu anakuwa na mipango yake kichwani kama anaenda kazini, na anahitaji utulivu kama anarudi kutoka kazini kwa sababu ya uchovu wa siku nzima na changamoto nyingine alizokutana nazo katika mizunguko yake. Hahitaji kusikia kelele za namna mnavyotongozana au jinsi ulivyomchongea jirani yako kwa mumewe au jinsi ulivyomshushua shoga yako mbele ya watu.*

**Danford Mitulinga- Mbagala**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Hata Amunike akiondoka, Stars itabaki ile ile tu




**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Timu ya Taifa ya Misri kutolewa kwenye hatua ya 16 Bora ya fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) kwa kufungwa bao 1-0 na Afrika Kusini, imeripotiwa kuwa Rais wa Shirikisho la Soka Nchini Misri (EFA), Hany Abourida, aliamua kumtimua Kocha Mkuu wa timu hiyo, Javier Aguire.

Halafu papo hapo na yeye mwenyewe Rais wa Shirikisho akatangaza rasmi kujiuzulu pamoja na Makamu wake, Ahmed Shobeir, kipa wa zamani wa Al Ahly na Misri.

Hii imetokana na aibu waliyoipata Wamisri kwa kuondolewa na timu iliyosonga mbele kupitia mlango wa uani "best looser" ya Afrika Kusini, huku wenyewe wakiwa ndiyo wenyeji wa michuano hiyo.

Kwa nchi yenye sifa kubwa ya soka kama Misri, kama si kutwaa ubingwa, angalau ingefika fainali au kutolewa hatua ya nusu fainali ndiyo kidogo mashabiki wangeelewa.

Na si tu kwamba Misri imefungwa na timu iliyoingia kwa staili ya 'best looser' Afrika Kusini, lakini tangu awali timu hiyo imeonekana haiko kwenye kiwango kizuri.

Wakati Misri kukiwa shaghala baghala, kuna tetesi ndani ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kuwa limefikia makubaliano ya kuachana na Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Emmanuel Amunike.

Na sababu inaelezwa ni hizo hizo kama za Wamisri, ni kufuatia kuboronga kwenye michuano ya AFCON ambapo Tanzania haikuambulia hata pointi moja.

Taarifa za ndani zinasema kuwa TFF kwa sasa ipo kwenye mchakato wa kumpata kocha mbadala wa muda atakayeinoa Stars kuelekea michuano ya CHAN.

Lakini hizi za TFF bado zinabaki kama tetesi, lakini Waswahili wana msemo wao unaosema 'lisemwalo lipo na kama halipo laja.'

Kwa jinsi Stars ilivyocheza AFCON, ninavyoona hata kama Amunike akitimuliwa sidhani kama kutakuwa na mabadiliko yoyote yale kwa muda mfupi kuelekea kwenye CHAN ambayo wanacheza wachezaji wa ndani tu.

Kwenye CHAN, Stars inakwenda kuwakosa wachezaji wachache ambao wanacheza soka la kulipwa nje ya nchi kama vile Mbwana Samatta, Simon Msuva na Himid Mao. Kwa kawaida Stars inaundwa zaidi na wachezaji waliocheza ligi ya ndani kwa asilimia 70 hadi 80.

Kama ni kweli Amunike atatimuliwa au kubwaga manyanga wala si mwarobaini wa Stars kufanya vizuri kwa mechi zijazo, bali ni mikakati madhubuti ifanyike na si kwa njia za mkato.

Inawezekana kinachotaka kufanyika ni kumwondoa ili kujiandaa kuwaita wachezaji ambao Amunike amekuwa hawataki kwenye kikosi chake.

Na huenda ikafanywa hivi ili kuwaridhisha na kuwarudisha kwenye mstari baadhi ya mashabiki ambao wamekuwa hawakubaliani na uteuzi wake na kuacha baadhi ya wachezaji ambao wao wanadhani kuwa wangeisaidia timu.

Hata kama Stars ikifanya hivyo na kushinda mechi ya kwanza, utakuwa ni ufumbuzi tu wa muda mfupi, lakini kuna tatizo kubwa kwenye soka la Tanzania ambalo inabidi litatuliwe na halihusiani kabisa na Amunike.

Inawezekana ni kweli Amunike akawa na matatizo yake kama binadamu, lakini si kweli kama kuboronga kwa Tanzania kunamhusu.

Ni miaka 39 sasa Tanzania ilikuwa inahaha kufuzu tu AFCON na miaka yote hiyo hakuwapo na Stars ilikuwa haifanyi vema, hiyo yote inaonyesha kuwa tatizo si yeye.

Tatizo linaanzia kwenye Ligi ya Tanzania, pamoja na kwamba inaelezwa kuwa ni maarufu na mvuto, lakini ukweli haina ubora na inaendeshwa kisiasa zaidi.

Mpaka ziondoke fikra za timu fulani zishinde ili ligi iwe nzuri, mashabiki wajae viwanjani, hiyo inasababisha udhaifu kwenye ligi kwa sababu mshindi aliyepatikana siyo aliyetakiwa.

Ligi ya Tanzania inadaiwa kutawaliwa na rushwa kwa baadhi ya mechi, lakini pia kupanga matokeo kwenye baadhi ya mechi.

Wachezaji wa Kitanzania wengi wao wameonekana hawana stamina wala pumzi wanapocheza dhidi ya wachezaji kutoka kwenye ligi zingine ndani ya Afrika na nje.

Kingine ni kwamba badala ya kutaka kupunguza wachezaji wa kigeni, tutumie nguvu nyingi kuwafanya wachezaji wa Tanzania watoke nje ya nchi ili kupata wachezaji wengi kwa ajili ya kuiboresha Stars.

Serikali nayo inapaswa ichangie kupatikana ubora wa Stars kwa kutengeneza miundombinu hasa ya viwanja, kwani viwanja vingi vya Kibongo ni vibovu na kufanya wachezaji badala ya kucheza mpira wawe wanapiga tu mpira, hivyo wanapofika kwenye michuano ambayo inahitaji ufundi wanashindwa.

Pia iangalie hata suala la uraia pacha kwa watu maalum na si kila mtu. Kuna wachezaji wengi wenye asili ya Kitanzania, lakini wana uraia na nchi nyingine na hawataki kuupoteza kwa sababu zao, lakini wanataka kuichezea Stars. Wachezaji kama hawa ni muhimu na Serikali inapaswa kuliangalia suala la uraia pacha kwa watu wenye vipaji maalum tu kama hawa ili nchi inufaike, kama ilivyo kwa Madagascar ambayo ina wachezaji wengi wenye uraia pia wa Ufaransa, walioifanya kushangaza wengi AFCON.

Haya yote na mengine ambayo sikuyaorodhesha yanaweza kuwa mwarobaini wa Stars kufanya vizuri na si kumtimua Amunike kwa sababu itafika wakati tutakuja kugundua kuwa Stars ni ile ile na tatizo liko pale pale.

**KABWELA** **NA FADHILI MOHAMMED**



# Hospitali maarufu hatihati kufungwa

INATOKA UK. 3

sababu shehena ya vifaa tiba hivyo ikiwasili, watapata vikwazo.

Mtawala huyo alisema hawauzi chochote au kufanya biashara, hivyo kama kuna mtu anasema wanafanya biashara apeleke ushahidi popote hata mahakamani.

Alisema hospitali hiyo ilifunguliwa kwa lengo la kusaidia wananchi ndiyo maana uongozi unaendelea na uboreshaji wa miundombinu na huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa tiba vyote.

Huduma za matibabu zinazopatikana katika hospitali ya Ikonda zimekuwa zikikimbiliwa na wananchi wa ndani ya nchi na nje na imekuwa msaada mkubwa kwa tiba ya magonjwa makubwa kabla ya kesi kubwa kuhamishiwa kwenye hospitali za rufani za kanda na Muhimbili.

Muuguzi katika chumba cha upasuaji, Joyce Malikila, alisema kufungwa kwa mashine za kisasa katika hospitali hiyo kumekuwa msaada mkubwa wa kutoa huduma nzuri.

"Mgonjwa akiwa katika hali mbaya tunaunganisha tu mashine. Sisi tunabaki kuwa waongozaji na kama anahitaji hewa ya nyongeza mashine inaonyesha ndipo sisi tunaongeza," alisema Malikila.

Hospitali hiyo ilifunguliwa na Rais (wakati huo) Nyerere Oktoba 7, 1968 lakini ilianza kujengwa tangu mwaka 1961 baada ya Chifu wa Wakinga (kabila linalopatikana wilayani Makete) kuomba mapadre wa Shirika la Waconsolata kujenga hospitali ili kusaidia watoto na kinamama kwa sababu kwa wakati huo wengi wao walikuwa wanafariki dunia kwa kukosa huduma za afya na njaa.

# Serikali yajipanga ununuzi wa vichwa, mabehewa SGR

**Na Futuna Seleman,** PWANI

SERIKALI imejipanga kununua vichwa vya treni 22, mabehewa ya mizigo 1,430 mabehewa ya abiria 60 ya kisasa na treni seti 5 zijulikanazo kama EMU.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, aliyasema hayo katika hafla ya kwanza la jaribio la treni ya uhandisi katika reli ya kisasa SGR juzi katika stesheni ya Soga Kibaha mkoani Pwani.

Alisema maendeleo ya ujenzi wa reli umefikia asilimia 56 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro na asilimia 12 kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora ambapo kazi mbalimbali za ujenzi zinaendelea.

"Kwa mujibu wa mkataba kipande cha Dar es Salaam-Morogoro kitakamilika mwishoni mwa mwaka 2019," alisema Kamwelwe na kuongeza:

"Ujenzi wa reli wenye jumla ya kilomita 722 Dar es Salaam hadi Makutupora unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unagharimu kiasi cha Sh. trilioni 7.2 ...reli hii itakapokamilika tunategemea kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa mizigo kupunguza uharibifu wa barabara kuongeza usalama wa safari na mizigo, na kupunguza muda wa safari."

Aidha, alisema Aprili 14, mwaka huu zoezi maalum la uunganishwaji reli lijulikanalo kitaalamu kama "flash butt welding" lilifanyika na sasa treni ya uhandisi imeanza kutembea juu ya reli ya SGR katika kipande kilichokamilika.

"Ijulikane hii ni treni ya Uhandisi (Engineering Train) itakayotumiwa na mkandarasi kama chombo cha kumwezesha kuendelea na ujenzi na kuitumia kubebea vifaa vya ujenzi, alisisitiza Kamwelwe.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania TRC, Masanja Kadogosa, alisema serikali imedhamiria kwa dhati kuirudishia Shirika la Reli uwezo wa ufanisi kwa hatua za kimataifa.

Alisema ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) unafanywa katika hatua mbalimbali ikiwamo ukataji wa miinuko, ujazaji wa mabonde kwa ajili ya ujenzi wa ruta la reli, ujenzi wa madaraja, makaravati, mifumo ya maji majengo ya stesheni na karakana na sehemu za kuchambulia mizigo.

Hatua nyingine ni uwekaji wa mifumo ya umeme yenye msongo wa kilovati 220 unaofanywa na Tanesco kwa ajili ya kupata umeme wa uhakika wa kuendesha treni na mfumo wa kuendeshea treni kwa msongo wa kilovati 25 unajengwa na mkandarasi, ujenzi wa mifumo ya mawasiliano pamoja na ishara kwa ajili ya kuongoza treni.



Ofisa Habari na Uhusiano wa Manispaa ya Ilala, Tabu Shaibu (wa pili kushoto), akikata utepe kuashiria kupokea msaada wa madawati 50 yenye thamani ya Sh. milioni tano kutoka kwa Meneja wa Tawi la Gongolamboto, Rehema Mwibura (kushoto) na Meneja Uhusiano Biashara za Serikali wa NMB, Faraja Kaziulaya (kulia), wakati wa makabidhiano kwa ajili ya Shule ya Msingi Yangeyange Msongola Manispaa ya Ilala, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atishia kumsweka ndani mkandarasi maji

INATOKA UK. 4

kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia Julai 2017 hadi Desemba, mwaka jana na kuongezewa tena muda hadi Juni 30, mwaka huu, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Waziri Mbarawa alisema mkandarasi huyo alitaka kumweka ndani muda wa siku tano ili ajifunze namna ya uharakishaji maana angetoka huko kazi ingeenda haraka kwa sababu angekuwa amejifunza kwa kuwa mkataba wanasainishwa na fedha nyingi wanachukua lakini mradi hauendi.

"Mkandarasi huyu mara kwa mara amekuwa akitoa ahadi za uongo kukamilika na wananchi wa maeneo ya Kagongwa na Isaka wana shida ya maji. Nimetaka kumweka ndani siku tano, lakini nimeona nimpe fursa aende kwa mkuu wa wilaya wakaandikishane. Aahidi mwenyewe kwani mimi nataka kufikia Agosti, mwaka huu, awe amekamilisha," alisema Waziri Mbarawa.

Alisema fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo ni Sh. bilioni 22 ambao umekuwa na awamu mbili. Awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa bomba kuu la usafirishaji maji kwa gharama ya Sh. bilioni 10 na awamu ya pili inahusu ujenzi wa mfumo wa usambazaji maji katika miji midogo ya Isaka na Kagongwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Kahama na Shinyanga (Kashwasa), Mhandisi Joshua Mgeyekwa, alisema mradi huo ulianza baada ya huduma ya maji iliyopo kutotosheleza mahitaji kwa miji ya Kagongwa na Isaka.

Kutokana na hali hiyo, alisema kumekuwa na upanuzi wa mtandao wa maji wa Ziwa Victoria na mpaka sasa mabomba yenye urefu wa kilomita 49.54 kati ya kilomita 52.9 yameshaazwa.

Mbunge wa Msalala, Ezeckiel Maige, alisema mradi huo ulianza mwaka 2017 na ulikuwa ukamilike mwaka 2018, lakini mkandarasi alipokuwa akitembelewa na viongozi, akiwamo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alisema angekamilisha ifikapo Juni, mwaka huu, lakini haikuwa hivyo.

Kutokana na tishio alilopewa, Oyao alikiri na kumweleza waziri kuwa atakamilisha mradi huo Agosti 18, mwaka huu, huku Waziri Mbarawa akisisitiza kuwa asipokamilisha ndani ya muda huo, awekwe ndani.

# Msaidizi wa Membe adaiwa kutekwa

INATOKA UK. 2

kuwa baada ya gari hilo kupita, lilikuja lingine aina ya Toyota Land Cruiser, likitokea nyuma ya gari la Allan.

"Hiyo Land Cruiser ilikuwa na rangi kama ya kaki, 'brown' au 'gold' hivi, nikamwambia Allan kuwa kuna gari lingine nyuma ili asogee mbele alipishe, Allan aliniambia mbona njia ni kubwa sana, nikamwambia asogee ili kuepusha ugomvi, akasogea. Aliposogea kama anarudi getini, lile gari nalo ikasogea, nikamwambia asogee tena ili kuepusha ugomvi. Aliposogeza gari alishuka na yule mtu kwenye Land Crusier naye akashuka," alisimulia.

Magreth alisema baada ya dereva wa Land Cruiser kushuka, aliangalia mbele na nyuma na akawauliza kwani vipi.

"Allan naye alimuuliza kwani vipi na mimi nilimuuliza mbona tumekupisha hujapita, wakati namalizia kujibu nilipomgeukia Allan, nikaona watu wamezunguka gari, wawili pembeni yetu, wawili nyuma yangu na wengine walikuwa kama saba na yule kaka wa kwanza. Wakamvamia Allan na kumpiga.

Allan alikuwa anasema Mage nisaidie, yule kaka wa kwanza akaninyooshea bastola, nikasikia mmoja anasema mchukue na huyo (yaani mimi).

"Huyu hakutii alichoambiwa na mwenzake, akaniambia nifanye haraka niingie ndani, nikanyata kurudi ndani sikufunga geti na komeo, nilipofika mlango wa kuingia ndani ya nyumba nikapiga kelele Allan ametekwa," alisema.

Magreth alisema walipotoka walikuta wameshaondoka ingawa kuna watu wa bodaboda walijitokeza na kueleza kuwa gari hilo lilipita mtaani hapo kama mara tatu.

"Tukio hili lilichukua kama dakika tatu hivi. Ila wakati tunatoka baa kuna bodaboda niliiona kama vile ilikuwa inatufuatilia lakini sikuitilia maanani, hawajachukua kitu waliacha gari, funguo, simu yake 'smart phone', simu yake ndogo ambayo alikuwa nayo ambayo ni ya laini yake ya Tigo, hata Polisi tumejaribu kuipiga haipatikani," alisema.

Membe alipotafutwa kupitia simu yake ya mkononi ili kuzungumzia suala hilo, ilikuwa haipatikani.

Tukio hili linatanguliwa na lile la Juni 24, la mfanyabiashara Raphael Ongangi, raia wa Kenya, kudaiwa kutekwa maeneo ya Oysterbay jijini Dar es Salaam na watu wenye silaha akiwa na mke wake, Veronica Kundya. Mfanyabiashara huyo alipatikana Jumanne iliyopita Mombasa, Kenya.

# WMA yageukia mizani ya madini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa vipimo nchini (WMA) umewataka wafanyabiashara na wachimbaji wa madini na vito vya thamani kutumia mizani ya kisasa iliyoidhinishwa ili kuepuka udanganyifu unaoweza kujitokeza.

Akizungumza katika maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaama (Sabasaba) yanayoendelea jijini Dar es Salaam mwishomi mwa wiki, Meneja wa Kitengo cha Habari wa WMA, Peter Chuwa, alisema mizani hiyo ya kidigitali inatumika kwa kuangalia usahihi wa hali ya juu wa madini husika kwa kuanzia kipimo cha juu hadi cha chini kabisa.

Alisema mizani hizo za digitali zina usahihi mkubwa kuliko mizani zingine za kawaida na inatumia hadi mawe madogo kabisa ambapo ukiweka katika mizani ya kawaida haiwezi kusoma chochote.

"Mizani hizi za digitali zina usahihi mkubwa kuliko mizani zingine, inatumia hadi vile vijiwe vidogo kabisa ambapo ukiweka katika mizani ya kawaida huiwezi kusoma wala huwezi kupata chochote.

"Tunafanya hivi tukijua madini ni bidhaa yenye thamani sana, hata ikipungua miligramu kadhaa tayari mteja anakuwa amepunjika, ndiyo maana tumependekeza aina za mizani na vifaa tunavyovitumia ni vya hali ya juu zaidi, ni vema basi wadau wote wavitumie.

Aidha, Chuwa aliongeza kuwa mizani hiyo ya kisasa imesambazwa katika maeneo yote ya migodini na katika vituo vyote vya kuuzia madini na vito vyote vya thamani nchini wakiwamo masonara.

"Kila mkoa kuna ofisi za Wakala wa Vipimo, kwa hiyo tunahakikisha kila kituo kina vifaa ambapo biashara hizi za madini zinafanyika, tunahakikisha hakuna biashara ya kupunjana kati ya muuzaji na mnunuzi bila kusahau kodi halali ya serikali," alisisitiza.



Mhasibu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Beatrice Kilimo (wa pili kushoto), akitoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira kwa mwananchi (kulia) aliyetembelea banda la baraza hilo, katika Maonesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam. kushoto ni Ofisa Mazingira Mwandamizi wa NEMC, Pendo Kundya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya DCB yajikita kwenye viwanda, kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha azma ya serikali ya awamu ya tano ya kuwa na uchumi wa kati unaotegemea viwanda ifikapo Mwaka 2025 inatimia, Benki ya Biashara ya DCB imeingia na mpango kabambe wa kuwiwezesha viwanda vya kilimo kwa kuja na bidhaa maalum ya DCB Sokoni ambayo inatoa suluhisho la kudumu kwa wakulima na wenye viwanda, huku ikilenga kuwawezesha wakulima na wafanyabiashara kiuchumi.

Bidhaa hii mpya itamwezesha mfanyabiashara mwenye azma ya kufungua viwanda vya kilimo kupata mikopo ya kuanzisha viwanda vya kilimo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa bidhaa hiyo uliofanyika pamoja na uzinduzi wa kiwanda kipya cha kukoboa mpunga cha mteja wake, Callington Kayuni, kilichopo katika kijiji cha Mlowo Mbozi Mkoa wa Songwe mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, James Ngaluko, alisema:

"Tunayo furaha kubwa leo kushiriki kwenye uzinduzi huu muhimu na wa tija wa kiwanda hiki kikubwa na cha kisasa cha kukobolea mpunga kilichojengwa kwa uwezeshwaji mkubwa wa Benki ya Biashara ya DCB, tunaamini kiwanda hiki kitakuwa mkombozi wa kweli kwa wakulima wanaofanya shughuli zao za kilimo katika kijiji hiki na vijiji vilivyopo karibu na hapa."

Alisema wa kuleta bidhaa hii mahususi ya DCB Sokoni, itawawezesha wafanyabiashara na wakulima sasa kufanya mapinduzi ya kweli kiuchumi kwa kutegemea kilimo pamoja na minyororo ya thamani kwani kupitia DCB wanaongezea thamani ya mazao ya mkulima.

Alizitaja njia ambazo bidhaa ya DCB Sokoni zitamwezesha mteja kukua ni pamoja na kujenga kiwanda, kununua na kusafirisha mazao kutoka shambani, kuuza mazao ghafi au kuchakata mazao na kuyaongezea thamani, usambazaji kwenda sokoni kwa wateja, ulinzi kutokana na bima ya maisha, kiwanda, pamoja na mazao ghalani katika kipindi chote cha mkopo, ununuaji wa nyumba ya makazi utakaowezesha kulipa taratibu kwa kipindi kirefu, ununuaji wa pembejeo kwa wafanyabiashara wa pembejeo na zana za kilimo, ubadilishaji wa fedha za kigeni zitokanazo na mauzo ya mazao na uwekezaji wa fedha kwa faida nzuri kupitia huduma ya DCB Lamba Kwanza.

Alisema uwezeshwaji wa viwanda vya kilimo kama ilivyo katika kiwanda hicho utachangia kwa kiasi kikubwa kasi ya uwekezaji kwa Watanzania. Vilevile uwezeshaji huu utasaidia pia kuongeza kiasi cha mazao ya biashara yanayouzwa nje ya nchi, mazao ya biashara kama pamba, kahawa, korosho na mengineyo, hivyo kuleta fedha za kigeni na kuinua pato la Taifa.

"Ni matumaini yetu wakulima na wafanyabiashara wa mkoa wa Songwe na maeneo jirani watakata mazao yao katika kiwanda hiki hivyo kuweza kupata chakula na biashara itakayowaongezea kipato na kuinua maisha yao," alisema na kuongeza:

"Benki inaunga mkono juhudi za serikali katika kuiwezesha sekta ya kilimo kifedha, sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi, baadhi ikiwa ni ukulima unaotegemea mvua za msimu na changamoto za upatikanaji wa masoko, kupitia DCB Sokoni ni imani yetu tutaweza kuleta ufumbuzi wa baadhi ya changamoto hizo."

Kayuni aliishukuru DCB kwa uwezeshaji wa kifedha alioupata uliowezesha ujenzi wa kiwanda hicho kutoka hatua ya awali mpaka mwisho kiwanda chenye uwezo wa kukoboa hadi magunia 350 kwa siku.

Hata hivyo alitaja changamoto ya masoko kuwa ni moja ya mambo yanayozorotesha ufanisi wa kiwanda kwani wakulima wanaoleta mpunga kukobolewa kiwandani hapo hutegemea kupata soko hapohapo la mchele, hivyo wapo mbioni kuomba mkopo wa kifedha kutoka DCB utakaowezesha suala hilo.

# Dawa ya mfumo dume yaelezwa

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa jamii ikiwa na uelewa juu ya dhana za jinsia, hali hiyo itasaidia kuondokana na mfumo dume.

Mfumo dume umekuwa ukitumika kutokana na jamii kutokuwa na uelewa wa haki zao.

Hayo yalisemwa na Monica John, ofisa habari kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao) alipokuwa akitoa mada kwa wadau wa semina za jinsia na Maendeleo (GDSS) zinazoandaliwa na TGNP Mtandao kila Jumatano.

"Jamii ikielewa jinsia, itawasaidia kujua haki sawa katika mgawanyo wa majukumu kati ya mwanamke na mwanaume," alisema.

Juma Bakari, mmoja wa washiriki katika mafunzo hayo, alisema mafunzo hayo yamemsaidia kujua jinsi na jinsia.

Alisema watu wengi wanajua jinsi na jinsia ni kitu kimoja, na kuwa ameweza kujua jinsi inasimamia nini na jinsia inasimamia nini.

Hafisa Hamis, alisema ikiwezekana uandaliwe utaratibu upelekwe katika shule ambapo wanafunzi wafundishwe masuala ya jinsi na jinsia.

# Faida za usajili biashara kimtandao

**Na Yasmine Protace,** KIBAHA

KAMPUNI zote na majina ya biashara zilizosajiliwa kwa mfumo wa kuandika kwa kutumia karatasi, sasa zinaingizwa kwa mfumo wa mtandao (ORS).

Hayo yalisemwa na mtaalamu wa mfumo wa mtandao, Francis Mwakalebela kutoka Brela.

Mwakalebela aliyasema hayo katika mafunzo ya siku mbili yaliyotolewa Kibaha kwa wanasheria, maofisa biashara na wafanyabiashara wa mkoa huo jinsi ya kutumia mfumo kwa ajili ya kusajili kampuni na majina ya biashara.

Alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuhakikisha walioyapata nao wanaenda kuwaelimisha jamii ambayo inafanya biashara jinsi ya kujisajili kwa kutumia mfumo ulioanza kutumika hivi sasa.

"Kampuni zote na majina ya biashara zilizosajiliwa kwa mfumo wa makaratasi sasa zinaingizwa kwa mfumo wa mtandao," alisema.

Aliongeza kuwa hiyo itasaidia kuzijua kampuni zote kupitia mitandao.

Alisema mtu ambaye hajasajili biashara ni vigumu kupata tenda, na kuwa ambaye atatumia jina la mtu kulifanyia biashara atakuwa anafanya makosa.

# Veta yatengeneza mashine bora ya kubangulia korosho

CHUO cha Ufundi Veta Songea mkoani Ruvuma kupitia kwa wanafunzi wake, kimetengeneza mashine ambayo itaweza kubangua korosho kwa ubora ili kumrahisisisha mtu kuondokana na ubanguaji holela.

Akizungumza na Nipashe katika Maonyesho ya 43 Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DTIF), mwanafunzi wa Veta Songea mkoani Ruvuma, Kandidus Nchimbi, alisema kuwa wameamua kutengeneza mashine hiyo iitwayo Cashewnutus Machine ambayo itasaidia ubanguaji korosho zisizochomwa wala kuchemshwa.

"Lengo la kutengeneza hiyo mashine ni kumwezesha mkulima ambaye anahusika na korosho asiwe na mchakato mkubwa kuiandaa korosho kumfikia mteja au mfanyabiashara," alisema Nchimbi. Alisema wanahitaji kufikia malengo yao hasa kuwafikia wakulima wa korosho ambao wapo pembezoni ili waweze kupata mashine hiyo kwa ajili ya kumrahisishia katika ubanguaji.

"Hii ni hatua ya kwanza katika utengenezaji wa mashine ya ubanguaji wa korosho, tuna mashine ndogo ila tunampango wa kutengeneza mashine kubwa ambayo itakuwa rahisi kwa mkulima kuendena na kaulimbiu ya Rais John Magufuli kuwa Tanzania ya Viwanda inawezekana," alisema Nchimbi.



Mkaguzi wa Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Nelson Nyabise (kulia) akitoa elimu juu ya utunzaji wa mazingira kwa mwananchi aliyetembelea banda la baraza hilo katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aita wawekezaji hifadhini

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantino Kanyasu amewaalika wawekezaji kutoka katika mataifa mbalimbali kuwekeza katika hifadhi za mazingira asilia kote nchini.

Uwekezaji huo ni katika ujenzi wa miundombinu, hoteli, kambi za utalii, vituo vya utafiti, utalii wa parachuti na mwingineo.

Alizungumza katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Kibiashara ya Dar es Salaam (DTIF), Kanyasu, alisema lengo ni kuhakikisha mtalii anapoingia hifadhini anapata huduma zote muhimu.

"Serikali tumeamua kuwekeza nguvu katika hifadhi zetu zote zinazobeba misitu, tumejipanga kujenga miundombinu madhubuti na ndio maana tumewaalika wawekezaji waje sasa, wajenge mahoteli, na tunataka hata huduma za kibenki na nyingine zote ziwepo ili mtalii anapoingia hifadhini asihangaike tena kwenda kutafuta huduma nje, tunataka akifika Msitu apate chakula, alale apate huduma za kifedha," alisema Kanyasu.

Alisema uboreshaji wa ikolojia katika hifadhi hususani za misitu ni muhimu katika kuhamasisha utalii.

Pia Kanyasu alisema katika msimu wa maonyesho hayo, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imeandaa safari za utalii kwa washiriki na ambao watafika katika maonyesho hayo kwa kuwapeleka katika hifadhi ya mazingira asilia ya Maghamba iliyopo Lushopo mkoani Tanga kuanzia Julai 12 hadi 14 mwaka huu. Ofisa Utalii, Mafunzo na Utafiti wa Hifadhi Asilia ya Maghamba, Samji Mlembe, alisema maeneo watakakowapeleka watalii wa maonyesho ya 43 ni katika vivutio vya jiwe la Mungu, Skyline, Grewal, mapango ya Wajerumani, vilele vya milima na vivutio mbalimbali vilivyopo ndani ya hifadhi. Pia Kanyasu alisema serikali imeweka mkakati wa kuhuisha mashamba yote ya hifadhi za misitu yaliyokuwa yameshaharibiwa.

Eneo jingine ambalo alisema serikali imeweka nguvu zake ni katika uzalishaji wa asali na kwamba tayari soko kubwa limepatikana Kenya.

# Sido yaongeza uwekezaji katika ubunifu

SHIRIKA la kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), limefanikiwa kuongeza idadi ya wawekezaji ubunifu na ajira kupitia mfumo wa kongani.

Akizungumza na Nipashe katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, Mkurugenzi Maendeleo ya Teknolojia na Uendelezaji Viwanda, Mhandisi Emmanuel Saiguran, alisema kongano hilo lilianza mwaka 2006.

Alisema Sido imelenga kuwasaidia wajasiriamali wa ndani ili waweze kufikia malengo yao.

Saiguran alisema Shirika la Maendeleo la Watu wa Japan (Jica), linasimamia kongani tano na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (Sida), linasimamia kongano 15, ambapo mbili zipo Visiwani Zanzibar na 13 Tanzania Bara.

Alisema kongani hizo ni mkusanyiko wa viwanda vilivyo karibu vinavyofanya shughuli zinazofanyika na kushabihiana vikisaidiwa na watoa huduma mbalimbali wanaolenga shughuli husika zilianza rasmi mwaka 2006.

"Kongani hizo zina viwanda 497, wanachama 3978 na zimezalisha ajira 11,934 tunashukuru zimeleta mwamko kwa wajasiriamali na wawekezaji wa ndani na nje pia," alisema Saiguran.

Saiguran alisema kongani hizo zipo katika Mikoa ya Manyara, Dodoma, Mwanza, Kilimanjaro, Shinyanga, Singida, Morogoro, Zanzibar, Pemba na Mbeya.

Alisema uwapo wa kongani hizo umeongeza ajira, uwekezaji, tiba, ubora wa bidhaa masoko.

Alisema kongani nyingi zinazalisha bidhaa za ngozi, mpunga, katani, nafaka, maziwa, alizeti na madini.

Saiguran alisema pia zimeleta chachu ya mahusiano wa kwa wao, viwanda vipya kuanzishwa ambapo pia Japan wamefadhili kupitia mradi wa Tanzania ili kuongeza tija katika uzalishaji bidhaa.

# Wakulima wa chai wapewa mbinu za uzalishaji

**Na Elizabeth Zaya**

WAKULIMA wa zao la chai wametakiwa kuendelea kulima zao hilo kwa wingi kuhakikisha soko lake linakuwa ndani na nje ya nchi.

Pia wametakiwa kulima aina mbalimbali za chai na kuacha mazoea ya kulima aina moja ya chai nyeusi badala yake walime aina mbalimbali ikiwamo chai ya maua.

Akizungumza jana jijini Dar as Salaam katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa, Meneja Masoko wa Kampuni ya Chai Bora, Awatif Bushiri, alisema kwa sasa wakulima wamekuwa wakilima aina moja ya chai hali inayowafanya watengenezaji wa majani ya chai kukosa kuweka aina nyingine ya chai na kutumia aina moja ya chai nyeusi.

"Wakati mwingine tunapata shida ya kutengeneza chai aina nyingine kutokana na wakulima wengi kulima chai aina moja na wakati mwingine huwa tunaamua kuagiza nje ya nchi chai za maua ambazo zinakuwa na harufu za matunda mbalimbali," alisema Bushiri.

Bushiri alisema zao la chai linasoko kubwa ndani na nje ya nchi, hivyo wakulima wakiongeza jitihada tutaweza kuzidisha kupiga hatua katika kufanya biashara na kujitangaza zaidi kwa nchi za nje.

"Sisi chai bora tumekuwa tukiuza bidhaa zetu hadi nje ya nchi na sasa tumefikia katika nchi tano ambazo tumekuwa tunauza chai yetu ikiwamo Ghana, Saudi Arabia, Afrika Kusini, Rwanda na Kenya," alisema Bushiri.

Kwa mwaka huu banda la Chai Bora limeshika nafasi ya kwanza katika kipengele cha chakula, dawa na vinywaji katika maonyesho hayo.

**HABARI ZOTE NA ELIZBETH ZAYA**

# Monduli walia upungufu wa magari kubeba wagonjwa

**Na Cynthia Mwololezi,** ARUSHA

UPUNGUFU wa magari ya kubebea wagonjwa uliopo wilayani Monduli umekuwa kikwazo kimojawapo kinachochangia kuwapo kwa mwitikio mdogo wa wananchi kuhudhuria hospitali kutokana na umbali.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Iddi Kimanta, wakati akikabidhi vifaa tiba vilivyotolewa na Taasisi ya Kumbukumbu ya Hayati Moringe Sokoine katika zahanati ya Monduli Juu kata ya Monduli Juu kwa lengo la kuboresha huduma za afya.

Kimanta alisema upungufu wa magari ya kutosha ya kubebea wagonjwa unachangia kuzorota kwa huduma za afya wilayani humo kutokana na wilaya hiyo kuwa kubwa, hivyo gari moja kushindwa kuhudumia wananchi wote kwa wakati mmoja hasa huduma za wajawazito.

"Tunaomba wafadhili mtufikirie kutununulia gari moja la kubebea wagonjwa ili tupate huduma za afya bila shida," alisema. "Tunawashukuru sana taasisi hii kwa kusaidia zahanati yetu kupata vifaa tiba ambavyo vitaboresha huduma za afya kwa wananchi wa jamii hii ya wafugaji na nimefurahi kuona mnaendeleza ndoto za Hayati Moringe Sokoine katika kusaidia wananchi katika masuala ya afya, elimu, mazingira, maji na kilimo na huu ni mfano bora wa kuigwa na jamii nzima," alisema Kimanta.

Naye Mjumbe wa Bodi ya wakurugenzi wa taasisi hiyo, Christine Sokoine, alisema, vifaa hivyo vimetolewa kwa udhamini wa kikundi cha wafamasia wasio na mipaka wa Ubelgiji kupitia taasisi hiyo kwa lengo la kusaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi hao.

Alisema taasisi hiyo ilishatoa kadi za bima ya afya 103 ambazo zimewanufaisha wananchi zaidi ya 600, ambao wamehudumiwa katika zahanati hiyo na kupata huduma mbalimbali za afya ikiwamo wajawazito kujifungua na huduma nyingine.

"Tangu taasisi hii tumeanza kusaidia kuboresha huduma za afya wilayani hapa ikiwamo vifaa hivyo vyote kwa pamoja vimegharimu Sh. milioni 8 na tumeahidi kuendelea kusaidia zaidi sekta ya afya ili kuondoa changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta hiyo," alisema Christine.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Lembris Kipuyo, alisema wataendelea kusaidia wananchi wilayani humo katika kuboresha huduma mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa wananchi juu ya kilimo bora ili waweze kujitosheleza katika kilimo na kufundishwa njia bora za kufuga kisasa.

Kwa upande wa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Titus Mmasi, alisema kuwa, taasisi hiyo inafanya kazi nzuri ya kuyaendeleza yale yote yaliyoanzishwa na Hayati Moringe Sokoine, na kwamba idadi ya wagonjwa wanaohudhuria kupata huduma za afya imeongezeka zaidi kutokana na kuboreshwa kwa huduma za afya.



Meneja wa Mradi wa Kilimo cha Shayiri wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Joel Msechu (kulia), akitoa maelezo kuhusu mbinu bora za uzalishaji kwa wakulima wa zao hilo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kilimo cha Shahiri iliyofanyika katika Kijiji cha Enguik, Kata ya Monduli Juu, mkoani Arusha kwa udhamini wa TBL. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tato, Polisi kuzindua kituo cha ukaguzi wa magari ya watalii

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

CHAMA cha Waongoza Watalii (Tato) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, wanatarajia kufanya uzindua wa vituo maalumu vya ukaguzi wa magari ya utalii.

Uzinduzi huo unatokana na kukamilika kwa matengenezo ya makontena manne na gari moja yatakayotumika kuhudumia watalii.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Fortunatus Muslimu, aliyasema hayo jana wakati akikagua makontena manne yaliofanyiwa ukarabati na kampuni ya Hanspaul ambayo yatatumika kama ofisi kwenye vituo maalum vya ukaguzi.

Alisema vituo hivyo vitaondoa malalamiko ya muda mrefu katika sekta hiyo na kusaidia kutoa huduma kwa watalii wanaotembelea vivutio mbalimbali katika Mkoa wa Arusha.

"Natamani uzinduzi huu ufanywe na Mkuu wa IGP, Simon Sirro, kwa kuwa wenzetu wa Tato na mdau wa maendeleo Hanspaul wamefanya mambo makubwa kwa kulisaidia Jeshi la Polisi kuimarisha utalii nchini na zoezi hili lisiishie tu hapa Arusha lifanyike pia mikoani," alisema.

Musilimu alipongeza kampuni ya Hanspaul na Tato kwa hatua ya kusaidia miundombinu hiyo katika sekta ya utalii, alitaka huduma kama hiyo ipelekwe pia mikoani kwa lengo la kuhudumiwa watalii ili kuimarisha sekta ya utalii nchini.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Hanspaul, Satbir Singh, alisema kampuni yake imefikia hatua ya kukarabati kontena hizo kwa lengo la kuimarisha sekta ya utalii nchini ili kuwaondolea kero watalii mbalimbali wanaotembelea vivutio nchini.

"Hizi kontena zitatumika kama ofisi na zitasaidia kutatua changanoto mbalimbali kwa watalii na sisi kama Hanspaul tunaunga mkono serikali yetu kupitia sekta ya utalii ili watalii waendelee kuja kwa wingi mchini," alisema Singh.

Naye Makamu Mwenyekiti Tato, Henry Kimambo, alisema Tato imeguswa na changamoto mbalimbali zinazowahusu watalii na kuamua kujitolea kutafuta miundombinu ya kontena na gari kwa ajili ya kuhudumia watalii ili kuboresha sekta hiyo.

Alisema gari hilo aina ya Land Cruiser limewagharibu zaidi ya dola 45,000 wakishirikiana na Jeshi la Polisi ambao wamelipia kodi ya gari hilo.

# Waomba udhibiti wa mbegu feki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI kwa kushirikiana na kampuni mbalimbali za uzalishaji mbegu nchini, wameombwa kudhibiti uwapo wa mbegu feki ambazo zimekuwa zikileta athari kubwa kwa wakulima na kusababisha wao kukata tamaa kuendelea kulima.

Hayo yalisemwa jana na mwenyekiti wa kikundi cha wakulima kijulikanacho Varemi, Yona Kitomari wakati akizungumza katika siku ya wakulima iliyoenda sambamba na utoaji wa elimu juu ya matumizi ya mbegu bora yaliyoandaliwa na kampuni ya utengenezaji na usambazaji wa mbegu ya IFFA .

Siku hiyo iliwashirikisha zaidi ya wakulima 100 kutoka kijiji cha Migandini Kata ya Maroroni wilayani Arumeru, ambapo wakulima hao walieleza changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni kuendelea kuwapo kwa mbegu feki sokoni.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wenzake, Kitomari alisema kumekuwapo na changamoto kubwa ya mbegu feki ambazo zimekuwa zikiuzwa na baadhi ya mawakala wa pembejeo za kilimo, hali ambayo huchangia kukosekana kwa mavuno ya kutosha na kumfanya mkulima kukata tamaa.

"Tunaomba sana serikali kwa kushirikiana na kampuni zinazozalisha mbegu kuhakikisha wanadhibiti uingizaji wa mbegu hizo feki kwani zinachangia kupoteza hari za wakulima kuendelea na kilimo na hata wakati mwingine kutokuwa na imani na mbegu nyingine kutokana na hasara ambayo tumekuwa tukiipata mara kwa mara," alisema Kitomari.

Meneja masoko wa kampuni ya mbegu ya kizalendo ya (IFFA) inayozalishaji na kusambaza mbegu aina ya Lubango na Kaspidi (chotara), Luhenda Yangole, alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wakulima kwa vitendo kupitia mashamba darasa ambayo wamekuwa wakilima mbegu hizo ambazo zinastahimili ukame na kuzalisha zaidi.

Yangole alisema wamekuwa wakiwatembelea wakulima kule walipo na kuwasambazia mbegu moja kwa moja kupitia vikundi vyao kwa lengo la kuepukana na changamoto ya uchakachuaji wa mbegu kabla ya kuwafikia wakulima, na kwamba wamewasaidia wakulima wengi kupata mbegu bora na kwa wakati.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Grace Solomon, aliwataka wakulima kuhakikisha wanabakiza kiasi kidogo cha mbegu walizotumia ili mwisho wa siku waripoti sehemu husika baada ya mavuno na kujua ubora wa mbegu walizotumia, kwani kwa kufanya hivyo wataweza kudhibiti uchakachuaji wa mbegu unaofanyika.

# Wajumbe 8 Baraza Ardhi watumbuliwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WATU wanane ambao ni wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kata ya Kia katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, wameng'olewa madarakani kupisha uchunguzi wa tuhuma za kupindisha haki na kushindwa kushughulikia masuala ya mirathi ya wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Yohana Sintoo, ametangaza kulivunja baraza hilo kwa mujibu wa Kifungu cha 23 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya Mwaka 1982.

Akitangaza uamuzi huo kwa niaba ya Sintoo, Mwanasheria wa Halmashauri hiyo, Hengelbert Boniface, alisema tayari ofisi yake imeagiza ofisa mtendaji wa kata hiyo kuunda baraza jipya litakalokasimu madaraka.

"Tumeshughulikia kero za mirathi inayohusu ardhi na mashamba 86 na kimsingi tumegundua kwamba mabaraza ya ardhi ya kata ni kama hayatusaidii, yanahusika kuendeleza migogoro kwa njia moja ama nyingine," alisema.

Alisema uamuzi wa kuvunja baraza hilo unatokana na kupokea malalamiko mengi yanayohusiana na Baraza la Ardhi la Kata ya Kia ambalo halikai kwenye vikao vyake halali.

Alipotafutwa kuzungumzia uamuzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alisema: "Haki ikipotoshwa taifa linakuwa hatarini, haki ikipotoshwa kwa watawala, ikapotoshwa pia mahakamani, taifa haliko salama."

Alisema ofisi yake ikimbaini mtu aliyenyang'anya haki za watu kwa nguvu na yenyewe itamnyang'anya kwa nguvu na kama ulitumia njia ya mkato kuipata na watatumia njia hiyo hiyo kunyang'anya ili kuondoa malalamiko.

Aprili mwaka huu, pia Ole Sabaya aliagiza kuvunjwa mabaraza mengine matatu yenye viongozi 24 kutokana na kutuhumiwa kupoka haki ya baadhi ya wananchi wasio na uwezo kiuchumi.



Diwani wa Kata ya Bomambuzi katika Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, akikabidhi Sh. milioni 5 kwa kiongozi wa kikundi cha vijana cha Bodaboda Mpesa Group kwa ajili ya miradi yao mbalimbali ya kujiingizia kipato. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waziri awatega wanaodaiwa kuuza mali za skimu ya maji

**Na Mary Mosha,** SAME

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, ameunusuru mradi wa skimu ya umwagiliaji wa mpunga wa Ndungu katika Wilaya ya Same kugawanyika vipande vipande, baada ya kuamuru waliouza mali za mradi huo kuzirejesha.

Menejimenti ya mradi huo iliuza kinyemela mali mbalimbali za mradi huo Juni Mosi, mwaka huu.

Naibu Waziri Mgumba aliagiza kurejeshwa kwa mali hizo jana, alipokwenda kukagua maendeleo ya mradi huo na kuzungumza na wakulima wanaoizunguka skimu hiyo.

Mgumba alisema ni marufuku vifaa vilivyomo kwenye eneo hilo la umwagiliaji kuchukuliwa na kuagiza vifaa vyote vilivyopigwa mnada virejeshwe hadi hapo serikali itakapo jiridhisha kwamba ni chakavu na kutoa kibali.

Baadhi ya wakulima, Yohana Karani na Cyphod Gomera, kwa nyakati tofauti waliiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kutatua changamoto hiyo, kwa kuwa inaonekana kudumaza shughuli za uzalishaji katika eneo hilo.

Mwenyekiti wa Mradi wa Wakulima wa Mpunga, Juma Kapongo, alimwambia Waziri Mgumba kuwa vifaa hivyo viliuzwa pasipo wao kushirikishwa na pia walizuiwa kununua kitu chochote katika mnada huo.

Alisema wameridhika na uamuzi alioutoa Naibu Waziri huyo, kwani vifaa hivyo havikuwa chakavu kama ambavyo Wakala wa Umeme (Temesa) waliwashauri Halmashauri ya Wilaya ya Same kuviuza.

Juni Mosi mwaka mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Same iliviuza vifaa mbalimbali vya skimu ya umwagiliaji ya Ndungu ikiwamo Isuzu Tank kwa Sh. milioni 20 na Isuzu Tiper kwa Sh. milioni 14.

Vingine ni kijiko (backhoe) kilichouzwa kwa Sh. milioni 18, katapila Sh. milioni 18 pamoja na katapila lisilo na injini ambalo limeuzwa kwa Sh. milioni 6.5 na rota Sh. milioni 3.

# Sababu ya migogoro kutishia vyama vya ushirika yatajwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MIGOGORO mingi ya vyama vya ushirika mkoani Kilimanjaro ambayo inatishia uhai wa sekta hiyo kutokana na kukithiri kwa matumizi mabaya ya fedha, wizi na kushindwa kusimamia rasilimali za vyama hivyo inatokana na jamii kutofahamu sheria.

Mhadhiri wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Grace Nolasko, aliyasema hayo jana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani ambayo hufanyika kila mwaka Julai 6.

"Kuna mambo mengi ambayo sheria inatoa mwongozo vizuri, lakini changamoto iko katika hatua ya utekelezaji. Yako mambo ambayo yana upungufu na hivyo yanahitaji maboresho zaidi ili vyama vya ushirika viweze kukua na kuendelea vizuri.

"Tumeona eneo mojawapo ambalo limekuwa na changamoto ni migogoro inayoendelea kufufukuta pamoja na utatuzi wa migogoro katika vyama vya ushirika."

Alisema vyama vingi vya ushirika Kilimanjaro vinakabiliwa na migogoro na baadhi ya vyama havijui hata vifanye nini japokuwa sheria iko wazi na imetoa utaratibu wa namna migogoro yake inatakiwa kutatuliwa na hasa kwa njia ya amani.

Kutokana na tatizo hilo, MOCU imeamua kuvitembelea vyama hivyo vya ushirika na kutoa elimu kuhusiana na mambo mbalimbali ikiwamo Sheria ya Ushirika, Namba 6 ya Mwaka 2013 na Kanuni zake za Mwaka 2015.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Endelevu ya chuo hicho na Mkuu wa Idara ya Ughani na Huduma za Jamii, Paulo Fute, alisema kauli mbiu ya ushirika duniani kwa mwaka huu ni ushirika kwa kazi zenye staha.

Kwa mujibu wa Fute, vyama ambavyo vimepata bahati ya kupigwa msasa kuhusu sheria na utatuzi wa migogoro ni Kilimanjaro Native Food Cooperative, Moshi Municipal Council Employed Saccos na Chama cha Ushirika wa mazao cha SAMA Amcos na Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Vijana Saccos vya Wilaya ya Siha.

Vingine ni vyama vya akiba na mikopo vya Muungano Saccos na Mamba South Amcos vya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na vyama vitatu vya Foo Amcos, Foo Daily Cooperative (wasindikaji wa maziwa), Foo Saccos na Kelamfua Mokala Saccos.

# Nipashe Spotika



SURA MPYA LIGI KUU BARA MSIMU UJAO UK.18



## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, juzi alionyeshwa kadi nyekundu baada ya kumfanyia faulo mchezaji wa Chile katika mashindano ya Copa America. Hii ni kadi ya pili ya Messi. Kadi ya kwanza nyekundu aliipata mwaka 2005 akiwa na kikosi hicho cha taifa lake.

# KAZI KAZI...

Beki wa pembeni wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Hassan Kessy (kulia), akijaribu kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Harambee Stars ya Kenya katika mechi ya Kundi C iliyochezwa kwenye Uwanja wa 30 June jijini Cairo. Kenya ilishinda mabao 3-2. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

## SOKA




# RAMSEY, RABIOT NA MAJINA MAKUBWA USAJILI WA BURE

**LONDON, England**

ILIPOFIKA Julai Mosi mwaka huu, maana yake wachezaji wote ambao wamemaliza mikataba yao na timu zao walikuwa huru kwenda popote.

Kati ya wachezaji hao ni Aaron Ramsey, Diego Godin na Adrien Rabiot tayari wamesaini mikataba na klabu mpya, huku Ander Herrera naye akiwa ametia saini pale Paris Saint-Germain.

Hapa tunawaangalia wachezaji ambao wamemaliza mikataba yao na wapi ambako wanaelekea.

**Aaron Ramsey**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Wales alimaliza muda wake wa kucheza pale Arsenal kwa miaka 11. Februari mwaka huu alisaini mkataba wa awali na mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus.

Wakati Massimiliano Allegri alipokuwa kocha pale Juventus alikubali Ramsey kujiunga na kikosi chake na sasa Maurizio Sarri akiwa amechukua mikoba ya kuwa kocha mpya, anaweza kumfanya kuwa kwenye kikosi chake cha kwanza cha Bianconeri.

Diego Godin

Alikuwa mhimili wa safu ya ulinzi ya Atletico Madrid tangu mwaka 2010, lakini Godin alitangaza kuondoka kwenye dimba hilo la Wanda Metropolitano Mei mwaka huu.

Inter walikuwa wanapewa nafasi kubwa ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 na Jumatatu akatangazwa rasmi kuwa ni mchezaji wao. Na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay amesaini mkataba wa miaka mitatu na miamba hao wa dimba la San Siro.

**Adrien Rabiot**

Huyu ni kiungo wa Ufaransa, ambaye hakupewa kabisa nafasi ya kucheza pale Paris Saint-Germain kwa mwaka wote 2019 kutokana na kukataa kuongeza mkataba na klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 tayari ameondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, na ametua kwa vinara wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus, ambao walitangaza kufikia makubaliano Jumatatu wiki iliyopita.

**Arjen Robben na Franck Ribery**

Baada ya kumaliza zama zao za kucheza pale Bayern Munich, Robben na Ribery wameondoka kwenye dimba la Allianz Arena.

Ribery amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na klabu na PSV, lakini Robben yeye ameamua kutundika daruga rasmi.

**Ander Herrera**

Manchester United walijaribu kumbakisha kiungo huyo wa zamani wa Athletic Bilbao, ambaye aliichezea mechi 132 miamba hao wa Ligi Kuu England tangu alipojiunga nao mwaka 2014.

Alikamilisha usajili wake kwenda pale Paris Saint-Germain wiki iliyopita na sasa ni rasmi mchezaji wa PSG.

Daniel Sturridge

Sturridge alikuwa mhimili mkuu wa Liverpool wakati wakiwa kwenye mbio za ubingwa wa msimu wa 2013-14, lakini majeruhi yakamfanya kutokuwa na nafasi nyingi yakucheza. Msimu uliopita alifunga mabao manne tu katika mechi 27 alizocheza kwenye mashindano yote.

Divock Origi ndiye alikuwa mbadala wa Sturridge wakati kocha, Jurgen Klopp alipoamua kumweka benchi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. Klabu kama Rangers ambayo inanolewa na gwiji wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard ndiko anakopewa nafasi ya kujiunga nao.

**Mario Balotelli**

Mchezaji wa zamani wa Manchester City, Liverpool na AC Milan, Balotelli alisaini mkataba wa miezi sita na Marseille Januari mwaka huu na alifunga mabao nane kwa miamba hao wa Ligue 1.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hajasaini mkataba wa kuendelea kukaa pale kwenye dimba la Velodrome, ingawa anapewa nafasi kubwa ya kurudi kucheza kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na anatajwa kwamba atatua pale Parma ambao wameonyesha nia ya kumtaka.

**JE, WAJUA?**



ARSENAL iko katika vita ya kuwania saini ya beki wa kushoto wa Real Madrid, Marcelo ambaye ana umri wa miaka 31. Mbrazil huyo analazimika kuondoka klabuni hapo baada ya kuelezwa kwamba hayuko kwenye mipango ya Zinedine Zidane.

# MICHEZO



## NJE YA UWANJA

### Magori awatuliza wanachama Simba

OFISA Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori, amesema kuwa "upepo mbaya" unaovuma katika klabu yao kutokana na kutofautiana kwa pande mbili za uongozi, utamalizika hivi karibuni.

Magori alisema kuwa wanachama na mashabiki wa Simba wanatakiwa kutulia, kwa sababu suala hilo linafanyiwa kazi na wanaamini ndani ya siku chache, hali ya utulivu itarejea klabuni hapo.

Kauli hiyo ya Magori imekuja siku chache baada ya kuwapo kwa sintofahamu iliyotokana na ujumbe wa "mafumbo" unaoandikwa na mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed Dewji "MO".

Taarifa zilizokuwa zinaelezwa jijini Dar es Salaam zinasema kuwa, kutokana na fukuto hilo, wakati wowote MO anaweza kutangaza kujiondoa ndani ya klabu hiyo, jambo ambalo linaashiria, Simba itarejea kwenye hali ngumu ya kiuchumi.



Taifa Stars

# REKODI YA 1980 AFCON ILIVYOKUWA NGUMU KWA STARS

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA imetolewa kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) imeshindwa kuifikia rekodi iliyoiweka yenyewe kwenye fainali za mwaka 1980 iliposhiriki kwa mara ya kwanza.

Stars imefungwa mechi zote tatu kwenye michuano ya mwaka huu ambayo ilifanyika Misri, ikiwa ni matokeo mabaya zaidi kuyapata, tofauti na waliyoyapata kaka zao miaka 39 iliyopita yakifanyika nchini Nigeria ambapo wao waliambulia pointi moja.

Tofauti ni kwamba fainali za mwaka huu 2019 zimeshirikisha jumla ya timu 24 kukiwa na makundi sita, wakati mwaka 1980 fainali zilishirikisha timu nane tu, kukiwa na makundi mawili.

Mwandishi wa makala haya anakuletea matokeo ya mechi zote sita za makundi, tatu zikiwa ni za kikosi kilichocheza fainali za mwaka 1980 na tatu zikiwa ni za kikosi cha msimu huu.

**1. Taifa Stars 1-3 Nigeria (1980)**

Tanzania iliweka rekodi ya kucheza kwa mara ya kwanza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika Machi 8, 1980 kwenye Uwanja wa Surulere, Lagos nchini Nigeria ikicheza na wenyeji wa michuano hiyo.

Stars ilikuwa kwenye Kundi A, ikiwa pamoja na timu za Misri na Ivory Coast.

Katika mechi hiyo, Stars ilikubali kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa vigogo hao ambao mwishoni mwa wiki walitinga hatua ya robo fainali baada ya kuwafunga Cameroon mabao 3-2.

Magoli ya wenyeji yalifungwa na mastraika hatari wakati huo, mastraika Mudashiru Batatunde maarufu kama Muda Lawal, Segun Odegbami na winga Emeka Onyedika, huku bao la kufutia machozi la Stars likifungwa na Juma Mkambi (marehemu), mchezaji aliyechaguliwa kutokea kwenye klabu ya Yanga.

**1. Taifa Stars 0-2 Senegal (2019)**

Baada ya miaka 39, Stars ilicheza mechi yake ya kwanza nchini Misri dhidi ya timu ya Senegal.

Mechi ilichezwa Juni 23 mwaka huu na Stars ilichapwa mabao 2-0, ikiwa imepangwa kwenye Kundi C.

Magoli ya Senegal waliwekwa nyavuni na Keita Balde na Krepin Diatta.

**2. Taifa Stars 1-2 Misri (1980)**

Mechi ya pili kwenye AFCON ya mwaka 1980, Stars ilikipiga dhidi ya Misri maarufu Mafarao, mchezo uliochezwa Machi 12.

Katika mechi hiyo, iliangukia tena pua kwa kuchapwa mabao 2-1.

Mabao hayo yalifungwa na Hassan Shehata ambaye kwa sasa ni kocha maarufu nchini humo, akiwahi kuzifundisha timu mbalimbali hata timu ya taifa, goli la pili likifungwa na Nour.

Stars ilipata bao la kufutia machozi likifungwa na Thuwein Ally, mchezaji aliyechaguliwa kutoka kwenye klabu ya Simba.

**2. Taifa Stars 2-3 Kenya (2019)**

Juni 27 mwaka huu, Stars iliingia kutupa karata nyingine kwenye michuano hiyo dhidi ya majirani zao Kenya.

Pamoja na kuonekana kama ushindi ungekwenda Tanzania, lakini dakika za mwisho, jinamizi liliendelea kuiandama Stars na kukubali kipigo cha mabao 3-2.

Mbwana Samatta na Simon Msuva wakifunga mabao kwa upande wa Tanzania, Michael Olunga akifunga mara mbili kwa upande wa Kenya na Johanna Omolo.

**3. Taifa Stars 1-1 Ivory Coast (1980)**

Hapa ndipo utofauti kati ya Stars ya mwaka 1980 na 2019 unapopatikana.

Machi 15, Stars iliweka rekodi ambayo haijafikiwa, ilipoilazimisha Ivory Coast sare ya bao 1-1 nchini Nigeria kwenye fainali hizo. Na ndiyo mechi iliyoifanya itoke na angalau pointi moja, kitu ambacho Stars ya 2019 haijakifanya.

Ivory Coast ndiyo iliyoanza kutangulia kufunga goli dakika ya saba likiwekwa wavuni na Koma Kobenan, lakini Thuwein Ally alisawazisha dakika ya 59.

**3. Taifa Stars 0-3 Algeria (2019)**

Kama Stars ingeshinda, basi ingeweza kuvunja rekodi ya kaka zao, lakini sare pia ingeweza kuweka rekodi kama ya mwaka 1980 ya kutoka walau na pointi moja, lakini ilijikuta ikirejea mikono mitupu, ilipofungwa mechi ya mwisho ya makundi kwa mabao 3-0 dhidi ya Algeria.

Mabao mawili yalifungwa na Adam Ounas, huku moja likifungwa na Islam Sulieman. Kwa matokeo ya mechi hizi zote ni kwamba, Stars ya mwaka 1980 ilipata bao moja kila mechi, huku ya mwaka 2019 ikipata mabao mawili kwenye mechi moja tu dhidi ya Kenya.

# Extra Time




# USAJILI MKUBWA UNAOSUBIRIWA KUTINGISHA ULAYA

**LONDON, England**

JULAI ni mwezi ambao unakuwa "bize" kwenye mchakato wa usajili kwa klabu mbalimbali duniani. Kipindi cha maandalizi ya msimu mpya kinakaribia kuanza na klabu zimekuwa zikiangalia namna ya kuboresha vikosi vyao kwa kusajili wachezaji wapya.

Kunakuwa na uvumi mwingi kuhusu wachezaji wakubwa na klabu ambazo wanahusishwa nazo kusajiliwa, huku pia fedha nyingi zikitumika. Hivyo hapa tunawaangalia wachezaji wakubwa ambao usajili wao unatajwa zaidi na wanaweza kusajili katika klabu mpya:

**4. Romelu Lukaku kwenda Inter Milan:**
**Klabu ya sasa:** Manchester United
**Ada yake**: Pauni milioni 75

Manchester United walitumia pauni milioni 75 kumchukua Romelu Lukaku kutoka Everton mwaka 2017. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ubelgiji alikuwa na mwanzo mzuri pale Manchester United, akifunga mabao 27 katika msimu wake wa kwanza klabuni hapo.

Hata hiyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alijikuta kwenye wakati mgumu katika msimu wake wa pili na alifunga mabao 13 tu katika mashindano yote msimu uliopita.

Pia alikuwa na wakati mgumu kupenya kwenye kikosi cha kwanza, huku kocha, Ole Gunnar Solskjaer akipendelea kumtumia zaidi Marcus Rashford.

Lukaku anataka kuondoka pale United katika kipindi hiki cha majira ya joto, huku Italia ndio kunaonekana ni sehemu ambayo anataka kwenda. Mshambuliaji huyo mara nyingi amekuwa akisema kwamba ana mapenzi makubwa mno na soka la Italia na siku moja anataka kucheza kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Klabu ya Inter Milan wapo tayari kumpa nafasi. Kocha mpya wa Inter Milan, Antonio Conte ametajwa kuwa ni shabiki mkubwa wa mchezaji huyo na anataka kumleta San Siro kipindi hiki cha majira ya joto.

Na mchezaji huyo ameripotiwa kwamba tayari amefikia makubaliano binafsi na klabu hiyo. Hata hivyo, Nerazzurri bado wapo kwenye mjadala wa makubaliano ya ada yake na Manchester United. Wanataka kumchukua mchezaji huyo kwa mkopo wa miaka miwili na huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa pauni milioni 70. Hata hiyo, United wanataka pauni milioni 75 kwa ajili ya kumuuza mchezaji huyo.

**3. Antoine Griezmann kwenda Barcelona:**
**Klabu ya sasa:** Atletico Madrid
**Ada yake:** Euro milioni 120

Antoine Griezmann anapanga kuondoka pale Atletico Madrid kipindi hiki cha majira ya joto baada ya mchezaji huyo kutangaza mapema msimu uliopita kwamba anaondoka. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 anaondoka Atletico kwenda Barcelona, ingawa kipindi cha majira ya joto kilichopita alisema anabakia hapo jijini Madrid.

Hata hivyo, Mfaransa huyo sasa amepanga kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto, na Barcelona ndio wanaotajwa kumnunua, baada ya kushindwa kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Ofisa Mtendaji wa Atletico Madrid, Gill Martin, alithibitisha kwamba Griezmann atakwenda Barcelona wakati wa mahojiano yake mwezi uliopita. Alisema, "Kumekuwa na sintofahamu kuhusu wapi Griezmann atacheza msimu ujao. Atachezea Barcelona."

Ripoti za hivi karibuni zimedai kwamba, Blaugrana wamekuwa wakisubiri ada ya Griezmann ya euro milioni 120 ili kumwachia mshambuliaji huyo.

Na inaonekana wazi kwamba, Barcelona watamchukua kipindi hiki cha majira ya joto na ada yake itakuwa ni euro milioni 120.

**2. Paul Pogba kwenda Madrid:**
**Klabu ya sasa**: Manchester United
**Ada yake:** Pauni milioni 150

Manchester United ilitumia kiasi cha pauni milioni 89 kumsajili Paul Pogba kurudi tena pale Old Trafford, na kumfanya kuwa mchezaji ghali zaidi duniani mwaka 2016. Hata hivyo, kipindi chake cha uchezaji pale Manchester United kimekuwa cha kupanda na kushuka, na wengi wanaamini kwamba kiungo huyo ameshindwa kufikia matarajio hasa kutokana na kiwango cha ada yake ya kununuliwa.

Mchezaji huyo ametamka hadharani kwamba anataka kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto, akisema kwamba ni wakati mwafaka kwake kutafuta changamoto mpya.

Kocha Zinedine Zidane anatajwa kwamba kuwa anavutiwa zaidi na mchezaji huyo na anapanga kumchukua ili akacheza pale Real Madrid kwenye dimba la Santiago Barnabeu ambako kwa sasa klabu hiyo ipo kwenye harakati za kuimarisha kikosi chake. Hata hivyo, Manchester United imekuwa haitaki kumuuza mchezaji huyo, lakini wakipata ofa ya pauni milioni 150 wanaweza kumwachia.

Madrid tayari imeshatumia kiasi cha euro milioni 300 kipindi hiki cha majira ya joto kwa ajili ya usajili na inaweza kuwa ngumu kuweza kufikia bei wanayoitaka United. Madrid wapo tayari kumtumia Gareth Bale kama chambo ya usajili huo, huku Manchester United wakiwa hawana mpango wa kumchukua nyota huyo wa kimataifa wa Wales kutua kwenye dimba la Old Trafford msimu huu.

**1. Neymar kwenda Barcelona:**
**Klabu ya sasa**: Paris Saint-Germain
**Ada yake:** Euro milioni 200

Neymar alikuwa mchezaji ghali zaidi duniani wakati aliponunuliwa na Paris Saint-Germain kwa euro milioni 222 mwaka 2017. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alitua pale kwenye jiji la Paris, huku wengi wakiwa na matarajio nae makubwa na waliamini kuwa anaweza kuwapaisha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, Neymar ameshindwa kufikia kile kilichotarajiwa na wengi tangu atue hapo PSG mwaka 2017 kutokana na mambo yake nje ya uwanja.

Mahusiano yake na klabu yanaonekana kuwa madogo zaidi na mchezaji huyo kwa sasa anataka kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto na Barcelona ndio inatajwa kuwa sehemu anayotaka kwenda.

Mchezaji huyo ameripotiwa kwamba amefikia makubaliano ya maslahi binafsi na Barcelona na yupo tayari kujiunga na Blaugrana hao. Paris Saint-Germain pia nayo imeonekana kuwa tayari kumwachia Mbrazil huyo.

## Nukuu

"Hakika ilikuwa ni miaka miwili bora sana kwangu, ndani na nje ya uwanja, Yanga ilikuwa ni sehemu ya familia yangu. Nitoe shukrani zangu za dhati kwa viongozi, benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki wote, kwa kuniamini na kuniunga mkono katika kila jambo. Ni mengi nimejifunza na ninaamini yatasaidia kunijenga zaidi kama mchezaji. Asanteni sana," **Ibrahim Ajibu, mchezaji mpya wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**



"Mungu wangu, wewe ni mrefu sana," maneno hayo **alisema Kocha wa Liverpool Mjerumani Jurgen Klopp** alivyokutana kwa mara ya kwanza na mchezaji mpya chipukizi wa timu hiyo, Sepp van den Berg (17), ambaye ametokea katika PEC Zwolle kwa ada ya pauni milioni 1.3.



"Nimeamua kufanya uamuzi ambao unaweka historia nyingine mpya katika maisha yangu," **Kiungo wa zamani wa Manchester City**, **Yaya Toure ambaye ni raia wa Ivory Coast,** alisema baada ya kutia saini mkataba mpya wa kuitumikia Klabu ya Daraja la Pili ya Qingdao Huanghai ya China.



# SURA MPYA LIGI KUU BARA MSIMU UJAO




Francis Kahata

**Na Adam Fungamwango**

USAJILI kwa ajili ya Ligi Kuu Bara msimu ujao na michuano mingine mbalimbali kwa klabu za Tanzania unazidi kushika kasi.

Klabu mbalimbali zipo kwenye pilikapilika za kutafuta wachezaji ambao wanaona wanafaa kuzitumikia kwa msimu ujao ambao unatarajiwa kuanza mwezi Agosti.

Pamoja na kwamba kutakuwa na wachezaji wale wale wa msimu uliopita wakiwa kwenye klabu zao au zingine, lakini Ligi Kuu msimu wa 2019/20 kutakuwa na sura mpya nyingi za wachezaji ambao watakuwa wakicheza kwa mara ya kwanza.

Ni wachezaji ambao wamesajiliwa na klabu za hapa nchini, kutoka nje ya Tanzania na watakuwa wakizichezea kwa mara ya kwanza kwenye klabu hizo na Ligi Kuu Bara.

Mwandishi wa makala haya anaorodhesha baadhi ya wachezaji ambao wataonekana kwa mara ya kwanza msimu ujao.

**1. Wilker Henrique da Silva - Simba**
Straika huyu ni ingizo jipya la Simba kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano mingine ya kimataifa. Amesajiliwa na klabu hiyo akitokea kwenye klabu ya Bragantino PA ya nchini Brazil. Mchezaji huyo ni raia wa Brazil.

**2. Melly Sivirwa- KMC**
Anacheza nafasi ya kiungo mkabaji, na amejiunga na klabu ya KMC FC ya Kinondoni jijini Dar es Salaam akitokea Vital'O ya Burundi. Kiungo huyo ambaye mashabiki wa Tanzania wanamshuhudia msimu ujao ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC).

**3. Issa Bigirimana - Yanga**
Ni straika raia ya Burundi ambaye anashuhudiwa akigusa kwa mara wa kwanza Ligi Kuu Tanzania kwa kuichezea klabu ya Yanga. Mchezaji huyo amesajiliwa akitokea klabu ya APR ya nchini Rwanda.

**4. Suleimani Ndikumana - Azam**
Kizazi cha sasa kitamshuhudia kwa mara ya kwanza straika Suleimani Ndikumana akicheza kwenye ardhi ya Tanzania. Ni mchezaji aliyewahi kuicheza Simba miaka ya 2006 hadi 2007, na hawajawahi kukanyaga tena.

Kwenye Ligi Kuu itakuwa ni kama sura mpya kwa kizazi cha sasa kwani, raia huyo wa Burundi amesajiliwa na Azam FC akitokea kwenye klabu ya Al Adalah ya nchini Saudi Arabia.

**5. Deo Kanda - Simba**
Baada ya marehemu, Patrick Mafisango, Mkongomani aliyekuwa na uraia wa Rwanda, itashuhudia Simba msimu ujao ikiwa na Mkongomani mwingine, Deo Kanda aliyechukuliwa kwa mkopo wa mwaka mmoja kutoka TP Mazembe. Huyu ni mmoja wa wachezaji wataopamba sura mpya kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

**6. Patrick Sibomana-Yanga**
Ni winga machachari aliyesajiliwa na Yanga akitokea Mukura Victory ya nchini Rwanda. Sibomana, raia wa Rwanda atakuwa akicheza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**7. Gerson Fraga Veira - Simba**
Ni Mbazil mwingine ambaye Simba itamtumia katika msimu ujao kwa ajili ya Ligi Kuu na mechi za kimataifa. Mchezaji huyo anayeweza kucheza nafasi ya beki wa kati na kiungo mkabaji, amesajiliwa klabu hiyo akitokea ATK ya India.

**8. Lamine Moro - Yanga**
Beki wa kati ambaye aliwahi kufika nchini na kucheza michuano ya Sportpesa akiwa na klabu ya Simba, amejiunga na Yanga na msimu ujao ataonekana kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Lamine ambaye alikuwa akicheza soka nchini Zambia ni raia wa Ghana.

**9. Tairone Santos da Silva - Simba**
Inaonekana huu ni mwaka wa Simba kwa Wabrazil, kwani huyu ni Brazil wa tatu sasa. Ni beki anayemudu kucheza namba za kati na pembeni na amesajiliwa akitokea klabu ya Atletico Cearense Fc ya nchini Brazil.

**10. Sadney Ukhrob - Yanga**
Straika huyu raia wa Namibia alishawahi kuja nchini na kuichezea Simba kwenye michuano ya Sportpesa na ikaonekana kama klabu hiyo hawana mpango naye, pamoja na mwenzake Moro.

Yanga imemsajili kwa ajili ya michuano mbalimbali msimu ujao na kuwa sura mpya kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

**11. Shiboub Sharaf Eldin-Simba**
Ni raia wa Sudan, anayeichezea pia timu ya taifa ya nchi hiyo. Ni kiungo mshambuliaji aliyesajiliwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara akitokea Al Hilal ya Sudan. Ni moja ya ingizo jipya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

**12. Juma Balinya - Yanga**
Ni mshindi wa kiatu cha dhahabu kwenye Ligi Kuu Uganda msimu uliomalizika. Mfungaji bora huyo Juma Balinya amejiunga na Yanga akitokea Polisi ya nchini humo.

Raia huyu wa Uganda awali alikuwa atue Simba, lakini alikataliwa na siku chache baadaye Yanga ikatangaza kumsajili.

**13. Francis Kahata - Simba**
Hili ni ingizo jipya kutoka nchini Kenya ambako msimu uliopita kulikuwa na ingizo kutoka huko, Meddie Kagere ambaye msimu huu amekuwa mfungaji bora.


Kahata naye ametokea klabu ya Gor Mahia kama Kagere, hivyo kuungana na mwenzake kwenye klabu ya Simba.

**14. Abdulaziz Makame - Yanga**
Makame ni ingizo jipya kwenye Ligi Kuu ya Bara akitokea Zanzibar. Ni kiungo mkabaji ambaye amejiunga na Yanga akitokea Mafunzo ya Zanzibar.

**15. Muharami Salum 'Marcelo' - Yanga**
Ni beki wa kushoto aliyesajiliwa na Yanga kutoka Malindi ya Zanzibar. Amesajiliwa kuziba pengo la Gadiel Michael ambaye ameonekana kuidengulia klabu yake na inasadikiwa kuwa ameshamalizana na Wekundu wa Msimbazi.

Muharami atakuwa ni ingizo jipya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**NAJUA WAJUA**



NAHODHA na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Mbwana Samatta, anawindwa na klabu mbalimbali za Ligi Kuu England ikiwamo Leicester City. Samatta bado ana mkataba na klabu yake ya KRC Genk inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji.

SOKA

# LAMPARD NA MFUPA WA WAKONGWE CHELSEA



**LONDON, England**

CHELSEA imemteua, Frank Lampard kuwa kocha mpya chini ya zama za Roman Abramovich baada ya Maurizio Sarri kwenda kwa mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus.

Lampard amepewa nafasi hiyo pale Stamford Bridge, akitokea Derby County ambako alikuwa akipata uzoefu baada ya kuichezea Chelsea kwa muda wa miaka 13.

Sarri hakuwa kwenye kiwango kizuri licha ya kuiongoza Chelsea kutwaa taji la Ligi ya Europa na kufika katika fainali ya EFL na kumaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Makala hii inakuchambulia makocha ambao wamepita chini ya zama za bilionea huyo wa Urusi, ambaye amekuwa hana utani wa kumfukuza kocha pale timu inapofanya vibaya.

**CLAUDIO RANIERI**

Wakati Abramovich alipoinunua Chelsea mwaka 2003, Ranieri ndio alikuwa kocha pale Stamford Bridge, lakini aliondoka mwaka uliofuata. Mtaliano huyo alishinda asilimia 61 ya mechi zote chini ya Abramovich wakati Chelsea ilipowanunua wachezaji kama Damien Duff, Joe Cole, Claude Makelele, Juan Sebastian Veron na Hernan Crespo na ilimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi, nyuma ya Arsenal. Chelsea pia ilifika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka huu na kipigo kutoka kwa Monaco kikahitimisha muda wa Ranieri.

**JOSE MOURINHO**

Alijitangaza mwenyewe kama 'Special One' wakati akitua hapo Chelsea. Na Mourinho akaiongoza Chelsea kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu pamoja na taji la EFL. Walitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na wakafungwa na Liverpool kwa bao la utata la Luis Garcia.

Blues hao walitetea taji lao msimu uliofuata, lakini msimu wa 2006-07 Manchester United wakalibeba. Mwanzo mbaya wa msimu wa 2007-08, pamoja na kutoka sare nyumbani na Rosenborg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kukamfanya Mourinho aondoke klabuni hapo.

Alirudi mwaka 2013 na Chelsea ikashinda taji la Ligi Kuu pamoja na lile la EFL. Lakini aliondoka tena Desemba 2015. Kwa kipindi chake alishinda mechi kwa asilimia 63.6.

AVRAM GRANT

Wakati Mourinho alipoondoka kwa mara ya kwanza pale Stamford Bridge, Abramovich alimleta Grant kushika mikoba ya Mreno huyo. Licha ya kutokuwa maarufu kwa mashabiki, Grant aliipeleka Chelsea fainali ya EFL na wakawafunga Tottenham na walimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Walitinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini akafungwa na Manchester United kwa changamoto ya mikwaju ya penalti. Na Grant akamaliza muda wake hapo Chelsea. Cha kushangaza ni kwamba ndiye kocha aliyeshinda asilimia nyingi zaidi ya mechi chini ya zama za Abramovich akiwa na asilimia 66.7

**LUIZ FELIPE SCOLARI**

Kocha wa zamani wa Timu ya Taifa ya Brazil, Scolari, ambaye aliwezesha kutwaa Kombe la Dunia, lakini alishindwa kumaliza msimu mmoja pale Chelsea baada ya kufukuzwa Februari mwaka 2009. Scolari alishinda asilimia 55.6 ya mechi wakati akiwa pale Chelsea.

**GUUS HIDDINK**

Wakati huo akiwa kocha wa Timu ya Taifa ya Urusi, Hiddink aliwasili kama kocha wa muda kuchukua mikoba ya Scolari na Chelsea ikatinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambako walifungwa na Barcelona. Walishinda taji la FA katika mchezo wake wa mwisho, lakini licha ya kuwa maarufu zaidi kwa mashabiki hakuweza kukaa.

Hiddink alionekana kuwa ndio chaguo la kurudi tena hapo wakati Mourinho alipoondoka kwa mara ya pili na aliisaidia timu kushinda mechi 12 bila kufungwa. Kwa kipindi chake Chelsea ilishinda mechi kwa asilimia 53.1.

**CARLO ANCELOTTI**

Ancelotti aliisaidia Chelsea mwaka 2009 kuwapiku Manchester United kutwaa taji la Ligi Kuu katika msimu wake wa kwanza, na akaongeza lile la FA. Lakini United iliifunga Chelsea michuano ya Ulaya na kwenye Ligi Kuu England msimu uliofuata na Ancelotti akaondoka akiwa ameshinda asilimia 61.5 ya mechi kwa kipindi chake.

**ANDRE VILLAS-BOAS**

Kama Mourinho, Villas-Boas alijiunga na klabu hiyo akitokea Porto lakini hakuweza kufikia mafaniko yake. Huku Chelsea ikimaliza ligi nje ya nne bora, alifukuzwa Machi 2012, huku akiwa na asilimia 47.5 ya ushindi, ikiwa ni asilimia ndogo zaidi chini ya zama za Abramovich hapo Blues.

**ROBERTO DI MATTEO**

Kocha mwingine wa muda ni Di Matteo alichukua nafasi ya Villas-Boas na Mtaliano huyo aliwawezesha kutwaa taji la FA kwenye fainali dhidi ya Liverpool. Di Matteo pia aliiwezesha Chelsea kuifunga Barcelona kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na penalti ya mwisho ya Didier Drogba iliwawezesha Chelsea kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich.

Di Matteo alipewa mkataba wa kudumu, lakini kufungwa kwao na Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi, kukamfukuzisha kazi. Kwa kipindi chake cha miezi nane hapo Chelsea alishinda asilimia 57.1 ya mechi zake.

**RAFAEL BENITEZ**


Kocha wa zamani wa Liverpool, Benitez, ambaye alikuwa na asilimia 58.3 ya ushindi kwa mechi pale Stamford Bridge, alikuwa mmoja wa makocha mabao hawakuwa maarufu kwa mashabiki. Lakini aliwawezesha kufuzu kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kulibeba taji la Ligi ya Europa wakati Chelsea ikiifunga Benfica mabao 2-1 kwenye mchezo wa fainali.

**ANTONIO CONTE**

Mtaliano mwingine, Conte alichukua nafasi baada ya kuwa na mafanikio makubwa kule Juventus na timu ya taifa ya Italia. Alishinda taji la Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza, lakini walifungwa na United kwenye fainali ya Kombe la FA. Conte alikuwa na asilimia 65.1 ya ushindi kwa klabu hiyo akishika nafasi ya pili nyuma ya Grant na msimu ujao atakuwa akiiongoza Inter Milan kwenye Ligi Kuu ya Italia.

**MAURIZIO SARRI**

Sarri hakuwa kwenye moyo wa mashabiki wa Chelsea, lakini aliwezesha kumaliza nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu England na aliiwezesha kutwaa taji la Ligi ya Europa. Sarri alishinda asilimia 61.9 kwa kipindi chake.



MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Nigeria 'Super Eagles", Ahmed Mussa, amesema kuwa endapo watafanikiwa kutwaa ubingwa wa Kombe la Mataifa Afrika mwaka huu, taji hilo atalitoa kama zawadi kwa aliyekuwa kocha wao marehemu, Stephen Keshi.

Nipashe
# Spotika



JULAI ni mwezi ambao unakuwa "bize" kwenye mchakato wa usajili kwa klabu mbalimbali duniani. Kipindi cha maandalizi ya msimu mpya kinakaribia kuanza na klabu zimekuwa zikiangalia namna ya kuboresha vikosi vyao kwa...

**Uk. 16-17**

# KWA NINI DYBALA HAWEZI KUWA SULUHISHO UNITED




Dybala

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United kwa sasa inapigana kuhakikisha inakijenga upya kikosi chake.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer alitangaza wazi kuwa vijana chipukizi wa Uingereza wanapewa nafasi kubwa kwao katika klabu hiyo na ameonekana kulitekeleza hilo kwa vitendo. Daniel James alisajiliwa wiki chache zilizopita kwa pauni milioni 15, huku pia akimtwaa Aaron Wan-Bissaka ambaye amejiunga na timu hiyo kwa ada ya pauni milioni 50.

Usajili wa wachezaji hao ni jitihada tu za United wakiwa kwenye harakati za kuhakikisha msimu huu angalau wanamaliza katika nne bora ya Ligi Kuu England.

Hawa wachezaji wawili sio ndio pekee ambao United wamekuwa wakiwaania. Kwani bado wapo kwenye harakati za kusajili wachezaji wengine ili kutua pale Old Trafford.

Kuna mchezaji wa kimataifa wa Argentina ambaye anachezea mguu wa kushoto naye anaonekana kutakiwa pale na klabu hiyo. Lakini sio Lionel Messi, bali ni Paulo Dybala. Lakini je, Dybala anaweza kuwa suluhisho la matatizo ya United?

Makala hii inakuchambulia sababu kwa nini Paulo Dybala hawezi kuwa suluhisho kwa Manchester United.

**1. Kushindwa kuthibitisha ubora wake**

Mwanzo Paulo Dybala, alikuwa akitajwa kama ndiye Lionel Messi mpya. Waargentina na mashabiki wa Ligi Kuu Italia, Serie A, walionekana 'kumshobokea' mno. Wengine walifikia hata kumfananisha mchezaji huyo na gwiji Maradona.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 hakuweza hata kuwa kwenye mbio za kuwania tuzo ya Ballon d'Or pale kwenye dimba la Allianz, na bado hajaweza kufanya lolote.

Alimaliza katika nafasi ya 15 kwenye mbio za kuwania Ballon d'Or mwaka 2017. Hajafika hata kwenye daraja la Antoine Griezmann, ambaye United pia walikuwa wanamtaka.

Sio ajali kwamba, Dybala mara zote amekuwa akishindwa kupenya kwenye kikosi cha kwanza cha Timu ya Taifa ya Argentina, kwani kiwango chake mara zote hakiwi katika daraja la juu.

**2. Thamani sawa na Neymar**

Kwa miaka michache iliyopita, fedha imekuwa inazungumza zaidi kwenye soka kwa dunia ya sasa. Pauni milioni 30 ni kama pauni milioni 5 kwa soka la sasa kwa klabu kununua wachezaji. Kwa sasa klabu zimekuwa zikitumia fedha nyingi mno kwa usajili wa wachezaji.

Kesi ya Dybala haiwezi kuwa tofauti. Ingawa hatangazwi sana, lakini Dybala bado ni mchezaji kwenye thamani kubwa zaidi pale kwenye Uwanja wa Allianz. Juventus ni klabu tajiri na fedha za United haziwezi kutosha kumnunua nyota huyo.

Ukiangalia umri wake ni mmoja wa wachezaji ambao ada yake haiwezi kuwa chini ya pauni milioni 200. Je, Manchester United wanaweza kuvunja rekodi ya kumnunua mchezaji huyo kutua Ligi Kuu England?

**3. Kulizoea soka la Uingereza**

Kwa miaka mingi tumeshuhudia majina makubwa ya wachezaji wakija kwenye Ligi Kuu England na wakashindwa kufikia matarajio ya wengi. Huwezi kusema kwamba hawakuwa na vipaji, lakini ukweli ni kwamba walishindwa kuzoea soka la Uingereza.

Soka la Uingereza ni la kutumia nguvu na la kasi, maana yake ni kwamba kama haupo imara na kasi ya miguu yako ni kwamba utashindwa tu. Bila shaka wengi watasema mbona David Silva na Juan Mata wameweza kulizoea soka hili wakati wao staili yao ya uchezaji ni taratibu. Je, Paulo Dybala ataweza kulizoea haraka soka la Uingereza? Kuna shaka kubwa hapo.

Hebu tumwangalie mchezaji mwenzake wa Argentina, Angel Di Maria kama mfano. Hakuna mtu yeyote anaweza kuwa na maswali juu ya kipaji cha mchezaji huyo wa Argentina, lakini je, anaweza kulizoea soka la England na ataweza kuchukua namba ya Ashley Young katika winga? Hilo ni jambo linaonekana wazi kuwa gumu kwake.

Soka la Uingereza sio la kila mchezaji, kwani staili yake inaonyesha wazi kuwa ni baadhi tu ya wachezaji ambao wanaonekana kufiti kwenye soka hilo na sio kila mtu.

Kwa kutumia fedha, United wanaweza kulipa kiasi chochote kumchukua mchezaji huyo, lakini ni wazi kwamba baadaye wataona wameramba garasa.

**USILOLIJUA**



KOCHA mpya wa Chelsea, Frank Lampard, amesema anamtabiria chipukizi, Callum Hudson-Odoi kwamba atakuwa mmoja wa wachezaji hatari hivi karibuni kutokana na kipaji alichokuwa nacho.



# Kijiji hatarini kukumbwa kipindupindu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Kijiji cha Isewe kilichopo Kata ya Chalangwa katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu kutokana na kaya nyingi kutokuwa na vyoo bora.

Hayo yalibainika wakati baadhi ya watendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kushirikiana na maofisa wa Shirika la Catholic Relief Service (CRS) walipotembelea kijiji hicho kwa ajili ya kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora ili kuepuka magonjwa.

Ofisa wa mradi wa ushirikishwaji vijana katika ujenzi wa vyoo bora kibiashara (YESB) kutoka Shirika la CRS, Mussa Mayenga, alisema kabla ya kuanza mradi huo walifanya utafiti katika kijiji hicho kwa kuzihusisha kaya 440.

Alisema walibaini kuwa kati ya kaya hizo ni kaya 351 hazina vyoo bora, kaya 59 hazina vyoo kabisa na kaya 30 ndio zenye vyoo bora, huku baadhi ya taasisi ikiwamo Shule ya Msingi Isewe nazo zikiwa hazina vyoo bora.

Alisema kufuatia hali hiyo, shirika hilo liliamua kuanza kuhamasisha wananchi kujenga vyoo bora kwa kuwatumia vijana waliopatiwa mafunzo maalumu na shirika hilo kwa kushirikiana na Chuo cha Veta pamoja na kufadhili ujenzi wa Choo bora katika Shule ya Msingi Isewe.

"Kipindupindu kinasababishwa na mtu kula kinyesi, sasa mtu asiye na choo bora ni rahisi kula kinyesi kwa sababu nzi ni rahisi kutoka chooni na kuja kutua kwenye vyakula na tukapata kipindupindu, sasa ni jukumu letu kujenga vyoo bora ambavyo vinajengwa kwa gharama nafuu na vijana wenu," alisema Mayenga.

Vilevile, aliwataka wananchi hao kushirikiana na vijana wanaojenga choo cha Shule ya Msingi Isewe kwa madai kuwa vifaa vyote vya ujenzi vinavyogharimu zaidi ya shilingi milioni 16 vimetolewa na shirika hilo na kazi ya wananchi ni kusaidia kuwasogezea mafundi vifaa.

Kufuatia hali hiyo Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Chunya, Esther Mwakalila, aliagiza kila mwananchi katika kijiji hicho kujenga choo bora kabla ya Julai 30 mwaka huu na kwamba ambaye hatatii agizo hilo atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema baada ya muda waliopewa wananchi hao kuisha watatembelea kukagua utekelezaji wake, huku akisisitiza kuwa hawataki kusikia tena kipindupindu wilayani humo.

Mwakalila alilishukuru CRS kwa kujitolea kutoa elimu kwa wananchi hao pamoja na kujitolea vifaa kwa ajili ya ujenzi wa choo katika Shule ya Msingi Isewe. "Kwa mujibu wa sheria tunatakiwa kuwapa siku 21 pekee ili mjenge vyoo bora, lakini mimi nimeamua kuwasaidia kwa kuwapa mwezi mzima ili mkamilishe kazi hiyo na uzuri mafundi wapo hapahapa kijijini kwenu," alisema Mwakalila.

Aidha, alisema operesheni ya kuwakamata wasio na vyoo itakapoanza watasalimika watu wasio na uwezo wakiwamo wazee na wale wanufaika wa Tasaf ambao watasaidiwa kwa njia nyingine.



Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Biashara DCB, Rahma Ngassa (kutoka kushoto waliosimama), Mkurugenzi wa Mikopo Midogo, Haika Machaku na Mkurugenzi wa Biashara wa DCB, James Ngaluko, wakiangalia mchele baada ya kutoka katika mashine ya kukoboa wakati wa uzinduzi wa kiwanda hicho. Habari Uk. 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wageni mbaroni madai kutorosha dhahabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

LICHA ya serikali mkoani Mbeya kufungua masoko mawili ya kuuzia madini mkoani humo, imebainika kuwa bado baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu wanaendelea kufanya biashara haramu ya kutorosha dhahabu.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki baada ya Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa kushirikiana na maofisa wa usalama wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) kuwanasa raia watatu wa kigeni wakitorosha dhahabu kwenda jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliwataja watu hao ni Clive Rooney (62) raia wa Ireland, Ross Chertsey (34) na Robert Charles (58) wote raia wa Uingereza.

Kamanda Mateli alisema watu hao walikamatwa Julai 3, mwaka huu alasiri wakiwa na vipande viwili vya dhahabu vyenye uzito wa gramu 1,044.95 ambazo zina thamani ya zaidi ya shilingi milioni 98.

"Watuhumiwa walikuwa na madini hayo wakitokea wilayani Chunya kuelekea jijini Dar es Salaam kupitia uwanja wetu wa Songwe tayari kuelekea nje ya nchi, maofisa wa uwanja waliwapekuwa na kuwakuta na dhahabu hiyo," alisema Matei.

Alisema watu hao wanaendelea kuhojiwa ili kujua ukweli zaidi wa jambo hilo pamoja na watu wengine waliokuwa wanashirikiana nao kwenye tukio hilo kwa ajili ya hatua zaidi za ksheria.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kutorosha madini na badala yake wayatumie masoko yaliyoanzishwa na serikali kuuza madini yao ili kuepuka mkono wa sheria.

Vilevile aliwataka Watanzania kuwafichua wanaotorosha madini ili wadhibitiwe kabla hawajafanikisha zoezi lao kwa maelezo kuwa lengo la serikali kuanzisha masoko ya madini ni kutaka kila anayefanya biashara ya madini alipe malipo yote yanayotakiwa.

Alizitaka mamlaka zote za serikali zinazohusika kwenye biashara ya madini kuhakikisha zinaendelea kuimarisha taratibu zao ili kuwadhibiti watoroshaji wa mali hizo.

# Vigogo watoleana maneno mbele ya RC

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe, Loema Peter na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Mnkondo Bendera, wametofautiana na kurushiana maneno mbele ya Mkuu wa Mkoa kutokana na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ikuti.

Viongozi hao walionyesha kutofautiana wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ya kukagua utekelezaji wa agizo la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi,) Selemani Jafo, la kuhakikisha ujenzi wa vituo vya afya unakamilika kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Katika Kituo cha Afya cha Ikuti ambacho ni miongoni mwa vituo vya mwanzo nchini kuanza kujengwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura, Chalamila alikuta chumba cha kuhifadhia maiti hakijakamilika licha ya muda uliotolewa na waziri kupita.

Akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Bendera alimchongea Mkurugenzi kuwa alikuwa amesimamisha ujenzi wa chumba hicho mpaka alipopata taarifa kuwa mkuu huyo atatembelea ndipo akawapeleka mafundi wakawa wanajenga usiku na mchana.

Alisema chumba hicho kutokamilika kwa wakati kumesababisha mashine ambazo zilinunuliwa kwa ajili ya kutumika kwenye chumba hicho kuwekwa nje kwa zaidi ya miezi mitatu kitu ambacho alidai ni hatari kwa madai kuwa mashine hizo zinauzwa bei kubwa.

"Haiwezekani watu baada ya kusikia Mkuu wa Mkoa anakuja ndio wanakazana kufanya kazi usiku na mchana, hatuwezi kuendesha serikali kwa mfumo huu na lazima tuache unafiki, Mkuu wa Wilaya anatoa maelekezo kwa Mkurugenzi lakini hayatekelezwi," alisema Bendera.

Akijibu maelezo ya Bendera, Loema alisema wakati huu sio wa kulaumiana, na kwamba endapo watakuwa wanafanya hivyo hawawezi kufikia malengo yanayokusudiwa.

Alisema halmashauri hiyo imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa kituo hicho ikiwa ni pamoja na kutoa shilingi milioni 50 kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa chumba hicho.

Alisema wameacha kutekeleza miradi mingine ya halmashauri na kuelekeza nguvu katika kukamilisha chumba hicho ili kianze kutumika na hivyo akadai kuwa marumbano sio mazuri hasa kwenye shughuli za maendeleo. "Sio mnasema sema tu, sisi tumetumia nguvu kubwa katika kuhakikisha chumba hiki kinakamilika haraka na kinaanza kutumika, lakini waliotuchelewesha ni Tamisemi japo sisi hatutaki kumnyooshea mtu kidole," alisema Loema.


Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Rungwe, Ezekia Mwakota, alimtaka Mkurugenzi kuacha kujitetea badala yake akiri kufanya makosa kwa kuchelewa kukamilisha ujenzi wa chumba hicho.

Alisema Mkurugenzi huyo huwa hatekelezi maagizo yanayotolewa na Mkuu wa Wilaya wala Halmashauri badala yake anatekeleza maagizo yanayotolewa na Mkoa pekee, kitu ambacho alidai sio sahihi kiutendaji.

Baada ya maelezo hayo, Chalamila alisema anafurahi kuona watumishi hao wanarumbana kwa kuelezana ukweli na mwafaka wa tatizo lililopo unapatikana kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Alisema anatoa siku saba kwa viongozi hao kukamilisha ujenzi wa chumba hicho kwa madai kuwa Rais Dk. John Magufuli anazo taarifa kuwa mashine zilizonunuliwa zipo nje. "Nikija baada ya Ijumaa nikikuta hakijakamilika nitamlipua mtu kwa hiyo hakikisheni mnafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kinakamilika na mashine zinafungwa," alisema Chalamila.

Kituo cha Afya cha Ikuti ni miongoni mwa vituo ambavyo vimejengwa kwa viwango vya hali ya juu na kukifanya kuwa miongoni mwa vituo vya mfano nchini.





# Wazee 10,290 jijini Dodoma wana vitambulisho matibabu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAZEE 10,290 kati ya 19,543 jijini Dodoma wamepatiwa vitambulisho vya wazee kwa ajili ya kuwasaidia kupata huduma za afya.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Ustawi wa Jamii wa jijini hapa, Rebeka Ndaki, wakati akisoma taarifa ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenye mkutano wa uzinduzi wa Baraza la Wazee Wilaya ya Dodoma.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 ambayo inayolenga kuwatambua na kuwapatia vitambulisho kwa kuwa wana mchango mkubwa kwa Taifa.

Ofisa huyo alisema vitambulisho 2,686 vipo kwenye hatua za mwisho kukamilishwa ili viweze kukabidhiwa kwa wazee.

"Mpaka sasa Halmashauri ya Jiji kupitia Idara ya Afya imewafikia wazee katika kata 33 kati ya 41 na kuwapiga picha wazee wapatao 12,979 sawa na asilimia 66.41 ya wazee wote waliotambuliwa ambapo tayari wazee 10,290 wameshapatiwa vitambulisho," alisema.

Alisema halmashauri hiyo katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2019 imetekeleza maelekezo ya serikali ya kutoa huduma ya matatibu bure kwa wazee 4,551 ambao walihudumiwa kwenye vituo vya afya kwa kutumia vitambulisho hivyo.

Akizindua baraza hilo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alitoa wito kwa jamii nzima kuwajali na kuwaenzi kutokana na mchango wao waliofanya katika kufanya kazi kubwa ya ujenzi wa Taifa na kuweka mazingira rafiki kwa vijana wa sasa kuishi kwa amani na utulivu.

"Wazee ni tunu ya Taifa, juhudi zao za muda mrefu ndiyo zimetufikisha hapa kama Taifa kwa hiyo ni lazima tuwaenzi kwa kila namna na mimi ofisi yangu iko wazi wakati wote kwa ajili ya kuwahudumia na kusikiliza changamoto zao," alisema Katambi.



Mafundi wakiandaa mabomba jana kwa ajili ya kusambazia maji katika vijiji vya Busungu, Bukima na Kwikerege, Musoma Vijijini mkoani Mara.
**NA MPIGA PICHA WETU**

# Bodaboda sasa wa ililia serikali matibabu ya ajali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuharakisha mpango wa bima ya afya kwa madereva pikipiki maarufu kama 'bodaboda' ili kusaidia waweze kumudu gharama za matibabu pindi wanapopata ajali.

Gharama za matibabu ni kati ya Sh. 500,000 hadi Sh. milioni 3 kulingana na majeraha ya mgonjwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili jijini hapa, madereva hao walisema pamoja na bodaboda kuleta neema ya ajira na kurahisisha usafiri, lakini ni janga la ajali ambalo linasababisha vifo na vilema vya kudumu.

Hata hivyo, walisema gharama za matibabu zimekuwa ni changamoto kwao na kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Mmoja wa madereva ambaye pia ni majeruhi wa ajali ya pikipiki, Adri Sahagagili, alisema gharama za matibabu yake ni kubwa hivyo kama angekuwa na bima ingesaidia kuepukana na gharama hizo.

"Unajua ajali inapotokea mtu unakuwa hujajiandaa, mimi nilipata ajali ya pikipiki ambayo imesababisha mguu wangu kuvunjika mara tatu hadi sasa zaidi ya Sh. milioni 2 zimetumika, ningekuwa na bima hapa ingenisaidia," alisema. Majeruhi huyo ambaye amelazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, alisema kuna umuhimu wa serikali kuharakisha mchakato wa bima ili kuepukana na gharama za matibabu.

Majeruhi mwingine, Petro Sang'a, alisema amelazwa kwenye hospitali hiyo miezi mitatu sasa hivyo na analazimika kuchangiwa na ndugu na jamaa ili aweze kumudu matibabu.

"Mpaka sasa nimetumia zaidi ya Sh. milioni 1.2 ndugu na jamaa wamekuwa wakinichangia, lakini pia nimelazimika kukata Bima ya Afya ya Jamii (CHF) ya Sh. 30,000 ambayo inanisaidia kwa matibabu madogo madogo na si kwenye matibabu makubwa," alisema.

Alisema kuna umuhimu wa kuwa na bima ambayo itaweza kusaidia watu waliopata ajali kumudu gharama za matibabu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo ambaye pia ni Daktari Bingwa wa Upasuaji, Ajali na Mifupa, Dk. Ernest Ibenzi, alisema hospitali hiyo kwa siku inapokea majeruhi wa ajali mbalimbali ikiwamo pikipiki 50.

Alisema kati yao majeruhi 12 hadi 17 kwa siku hufanyiwa upasuaji kulingana na majeraha waliyoyapata kwenye maeneo mbalimbali ya mwili.

"Wengi wanaokuja huwa wamevunjika miguu, mikono na kuumia kwenye vichwa, hawa wagonjwa huwa wengi wanakuja unakuta ameumia kwenye kichwa huoni chochote lakini ndani ubongo unakuwa umeathiriwa ikiwemo kuvia damu," alisema.

Akizungumzia gharama za matibabu, Dk. Ibenzi alisema kwa wanaovunjika miguu wanagharimu takribani Sh. milioni 1.5, mikono kati ya Sh. 500,000 hadi 600,000, huku waliomia vichwani ni Sh. 800,000 na hutegemea na kiwango cha mvunjiko.

Alisema kwa wasio na uwezo wa kumudu gharama hizo hutibiwa kwa utaratibu wa msamaha ambapo serikali hurejesha gharama zao kwenye hospitali husika.

"Serikali hutoa msamaha wa muda, lakini huku mgonjwa akiendelea kutibiwa, huu msamaha sio bure serikali hurejesha fedha hizi kwa kuzirudisha kwenye hospitali, anasema gharama hizo ni pamoja na vyuma wanavyowekewa waliovunjika miguu ambapo kwa mfupa wa paja chuma chake kinagharimu Sh. milioni 1.5," alisema.

Dk. Ibenzi alisema kwa wale wanaotakiwa kubadilishiwa nyonga gharama yake hufikia kiasi cha Sh. milioni 2 hadi 3.

"Hawa majeruhi ambao mivunjiko sio mikubwa wanakaa hospitali kwa siku 7, lakini wale ambao wamevunjika sana wanakaa hadi miezi 6 hospitali, mwenye shida ya kichwa anatibiwa hadi apate fahamu, kwa hiyo unaona ajali hizi zinasababisha kushindwa kuendelea na shughuli zao za kiuchumi," alisema.

Mganga huyo alisema mpango wa bima kwa watu wote utakuwa suluhisho kwenye gharama za matibabu ya ajali.

## Watumishi waelekezwa kufanya usafi wa Jumamosi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WATUMISHI wa taasisi za serikali wamedaiwa kutoshiriki kikamilifu katika zoezi la kufanya usafi ambalo hufanyika kila Jumamosi.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Idara ya Mazingira na Mdhibiti wa Taka ngumu Jiji la Dodoma, Dikson Kimaro, baada ya kumalizika kwa usafi eneo la Uwanja wa Ndege.

Kimaro alisema watumishi hao wamekuwa ni changamoto kubwa katika kushiriki shughuli za usafi licha ya suala hilo ni agizo la serikali kwa watu wote nchini.

"Usafi umekuwa ukifanywa kila Jumamosi ukiacha ya mwisho wa mwezi, lakini watumishi wa serikali hawatoki kufanya usafi, wanaiachia jamii inayowazunguka jambo ambalo linarudisha jitihada za serikali za kuweka mazingira safi," alisema.


Aliwataka kuonesha mfano ili wawe na ujasiri wa kuwahimiza wananchi kufanya usafi na kutii sheria pasipo shuruti.

Alisema mbali na Dodoma kuwa Jiji, pia ni Makao Makuu, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi mkazi na ambaye siyo mkazi kuhakikisha anatunza mazingira na kulifanya jiji kuwa safi muda wote.

"Hii itawezesha pia kupambana na magonjwa ya mlipuko ambayo yanaweza kujitokeza kama hapatakuwapo na usafi wa kutosha hasa magonjwa ya kuhara na mazalia ya mbu ambayo yanaweza kusababisha malaria au dengue," alisema Kimaro.

Aliongeza kuwa kwa sasa katika jiji hilo hakuna changamoto ya ukosefu wa vyoo bora kwa wakazi wa mijini tofauti na maeneo ambayo bado hayajapimwa na wananchi kurasimishwa.

Pia alitaka jamii kuhakikisha inajenga vyoo bora na kushiriki kikamilifu katika utunzani wa mazingira.



HABARI ZANZIBAR



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, akizungumza na wakazi wa kijiji cha Mkwakwa Mafleta juzi. kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo na kushoto Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa Wilaya ya Muheza, Salehe Sabasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Balozi Seif asisitiza nidhamu matumizi ya fedha za serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Mahonda, Balozi Seif Ali Iddi, amesema upo umuhimu wa kuendelea kuziheshimu fedha zinazotolewa na serikali kwa lengo la kufanikisha miradi ya maendeleo na kiuchumi kwenye majimbo inafanikiwa kupitia mifuko ya majimbo iliyoanzishwa.

Balozi Seif ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais, alisema serikali imeamua kutenga fedha maalum za kuunga mkono miradi ya wananchi kupitia kamati zao za maendeleo ya jimbo na kamwe haitapendelea kuona baadhi ya watu au kamati zinakwenda kinyume cha utaratibu huo uliowekwa.

Balozi Iddi alisema hayo wakati alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo na ustawi wa jamii katika jimbo lake.

Alisema wananchi wameshaonyesha imani kubwa kutokana na mfumo huo uliowekwa na serikali, na kuwa mfuko wa jimbo umekuwa tegemeo la kusaidia kukwamuka baadhi ya miradi waliyoianzisha majimboni.

Balozi Iddi aliwapongeza wananchi wa Shehia ya Kinduni na kuushukuru uongozi wa kamati ya mfuko wa Jimbo la Mahonda kwa jitihada walizochukua za kujiondoshea changamoto zinazowakabili ikiwamo tatizo la barabara ya Kichungwani-Shule ya Msingi ya Kinduni.

Aliwaahidi kwamba atafanya jitihada za kuzungumza na kuuomba uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji usaidiae kuiboresha barabara hiyo ili iweze kutoa huduma nzuri ya usafirishaji.

Akizungumzia bajeti za miradi ya maendeleo majimboni, aliwataka wasimamizi wa miradi hiyo kuhakikisha kwamba kiwango kinachokubalika katika mipango ya miradi lazima iheshimike.

Alisema ipo miradi inayotengewa fedha kutokana na utekelezaji wake kukwama kutokana na mabadiliko yanayofanywa na baadhi ya wasimamizi na kupelekea kushindwa kukamilika. Mbunge wa Jimbo la Mahonda, Bahati Abeid Nasir, alisema juhudi zitaendelea kuchukuliwa na uongozi wa jimbo katika kuona miradi ya maendeleo inakamilika. Bahati alitolea mfano miradi ya ujenzi wa majengo mapya ya shule katika jimbo hilo itaendelea kuungwa mkono licha ya kumalizika kwa awamu ya kwanza ya fedha za mfuko wa jimbo.

Hata hivyo, alieleza kwamba ukamilishwaji wa ujenzi wa majengo hayo utafanywa baada ya kuingizwa kwa fedha nyingine za jimbo.

Naye Sheha wa Sheha ya Kinduni, Ali Ameir Khamis, alisema mradi huo wa uwekaji wa kifusi katika barabara ya Kichungwani hadi Shule ya Msingi ya Kinduni umeanza kutokana na shida kubwa ya usafiri waliyokuwa wakiipata wananchi.

## Jumuiya CCM zapewa mbinu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA za Chama Cha Mapinduzi (CCM) zimetakiwa kuzidisha juhudi katika kufanya kazi za kukiimarisha chama hicho.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Mkoa wa Magharibi Unguja, Mohamed Rajab Soud, wakati akiwahutubia wajumbe wa mkutano wa Baraza la Jumuiya ya Wanawake (UWT) Mkoa wa Magharibi Unguja.

Alisema jumuiya za CCM licha ya kufanya vyema katika majukumu yake ya kila siku bado zinatakiwa kuongeza kasi ya kiutendaji na kiubunifu ili kuhakikisha chama ndani ya mkoa huo kinaimarika kisiasa, kiitikadi na kiuongozi.

Kupitia mkutano huo, aliwataka wanawake hao kuwa wanategemewa na chama hicho katika harakati mbalimbali za kisiasa, hivyo wanatakiwa kutumia uwezo wao wa kisisa na kitaaluma ili kuhakikisha inapata ushindi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Alisema wanawake hao wanapaswa kuongeza juhudi zao kutekeleza kwa wakati mwafaka majukumu kadhaa vikiwamo vikao kwa mujibu wa katiba ya jumuiya hiyo.

Alisema viongozi na wanachama kila mmoja kwa nafasi yake wanatakiwa kuwaeleza wananchi katika maeneo yao utekelezaji wa Ilani ya CCM unaotekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli pamoja na wabunge, wawakilishi na madiwani.

Aidha, alisema mkoa huo upo katika maandalizi ya kutekeleza kwa vitendo kampeni ya Magharibi ya Kijani kwa kuhakikisha mkoa huo unakuwa ni ngome imara ya CCM kisiasa.

Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa huo, Zainab Ali Maulid, alisema jumuiya hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza kazi mbalimbali za kuleta maendeleo

# Waziri: Zanzibar ijitangaze vivutio vyake utalii kimataifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, amesema umefika wakati kutengeneza 'brand' (alama) ya Zanzibar kuwa ni kituo kikubwa cha utalii duniani.

Aliyasema hayo katika hafla ya kuipongeza hoteli ya Essque Zalu Zanzibar iliyoko Nungwi Kaskazini Unguja, baada ya kutwaa tuzo ya ubora duniani nchini Mauritius.

Waziri huyo alisema bidhaa za viungo vya Zanzibar, fukwe, Mji Mkongwe wenye historia ya pekee, magofu na mambo ya kale, sasa washika bango la utalii waitaje Zanzibar kwa haiba yake kila fursa inapopatikana.

Alisema Julai 25, mwaka huu, anatarajia kuzindua kamati ya taifa inayosimamia mchakato wa kutengeneza alama (Brand) hiyo itakayojumuisha wadau wa utalii na mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Jina la Zanzibar limekuwa midomoni mwa watu wengi kutoka nchi mbalimbali duniani, ambao hata kama hawajawahi kuja hapa, wana hamu kubwa ya kuijua nchi yetu, na ikitajwa tu athari zake huonekana katika nyuso na kauli zao," alieleza.

Waziri Kombo alisema kuna vivutio vingi vya utalii nchini ambavyo vimetangazwa vya kutosha na kuwavutia watalii wengi zaidi na kuliweka juu jina la visiwa vya Zanzibar. "Kuna namna nyingi za kuitaja Zanzibar, kwa mfano tunaweza kuwa na huduma ya 'Zanzibar massage' inayotumia mafuta na viungo vya Zanzibar pamoja na vitu vingine, badala ya kutumia majina ya nchi nyingine, kama vile "Thai Massage," alisema.

Alieleza kuwa tuzo kadhaa ambazo Zanzibar imepata katika miezi ya karibuni, ni kielelezo cha hazina zilizojikita nchini ambazo zinaweza kuvijengea jina zuri visiwa vya Unguja na Pemba, akitoa mfano wa tuzo iliyonyakuliwa na Chumbe Island Coral Park kwa kuwa kinara wa vituo 100 endelevu katika maonyesho ya utalii jijini Berlin, Ujerumani.

Aliupongeza uongozi wa hoteli ya Essque Zalu na wafanyakazi wake wote, akisema jitihada zao, mapenzi na dhamira ya dhati ndio iliyowezesha kunyakua tuzo hiyo miongoni mwa nchi mbalimbali zikiwamo za visiwa kama Mauritius, Seychelles na nyingine.

Aliwahakikishia wawekezaji wote wa sekta ya utalii, kwamba serikali itaendelea kushirikiana nao kwa kuwafuata na kujumuika pamoja na wale watakaofanikiwa kushinda tuzo za kimataifa ikitambua ushindi huo ni hadhi na fahari kubwa kwa Zanzibar ambayo kwa sasa inategemea zaidi utalii katika kukuza uchumi wake.

Meneja Mkuu wa hoteli hiyo, Cyrus Mutuota, alisema hafla ya kutunuku tuzo za 'World Travel Awards' (WTA) ilifanyika Juni 1, 2019 nchini Mauritius na kuwa hoteli yake imeibuka ya kwanza miongoni mwa nyingi za nchi mbalimbali.

Aliishukuru Serikali ya Zanzibar na Kamisheni ya Utalii kwa msaada na ushirikiano mkubwa wanaotoa kwa wawekezaji wa sekta ya utalii.

## NMB kurasimisha huduma za serikali

**Na Romana Mallya**

BENKI ya NMB imetanganza kutekeleza mifumo ya malipo ya kidijitali nchini ikiwa ni sehemu ya juhudi ya kufanya kazi na serikali kwa ajili ya kurahisishia utoaji huduma zenye usalama, nafuu, rahisi na uhakika katika kukusanya kodi na malipo mbalimbali ya serikali.

Kauli hiyo iliyolewa jana jijini Dar es Salaam na MKuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali wa NMB, Vicky Bishubo, na kwamba mfumo huo utawahusu wateja wa benki hiyo na ambao siyo wateja.

Kwa hivi sasa zaidi ya mamlaka za serikali za mitaa 180 nchini kote ambazo zimeunganishwa na mifumo mbalimbali ya mtandao wa kielektroniki ambapo benki inasaidia ukusanyaji wa kodi.

Halmashauri nyingine ambazo zimeongezeka katika kutumia mifumo ya kulipia huduma mbalimbali kupitia NMB ni pamoja na Manispaa ya Ubungo, Ilala, Temeke na Kigamboni. Mifumo ya malipo na ukusanyaji wa kodi inayotolewa na NMB inawezesha walipakodi kulipa kodi zote kwa urahisi, huku ikizipa serikali za mitaa uwezo wa kukusanya kodi kwa ufanisi.

"Hapa NMB tumekuwa tukiboresha na kuweka njia bora zaidi kwa kuziunganisha serikali za mitaa katika kutoa huduma za kifedha jumuishi ambazo ni rafiki kwao.

"Tumeunganisha mifumo yetu na mfumo wa kukusanya mapato ya serikali kwa njia ya kielektroniki (Government Electronic Payment Gateway – GePG). Hii itamwezesha kila mmoja kuweza kulipa kodi kwa urahisi, popote alipo kwa kutumia simu ya mkononi," alisema.

"Tunajiona kama mdau na mshiriki muhimu wa serikali na ndio maana tunajikita zaidi kuweka mifumo inayochangia kupunguza au kuondoa changamoto za sasa na za baadaye kwenye mamlaka za serikali za mitaa zilipo kwenye ukusanyaji wa kodi na pia mahitaji yao ya malipo," aliongeza kusema.

NMB itaendelea kuwa kinara wa kutoa huduma za kifedha bora zilizo na usalama, rahisi na zenye uhakika kwa wateja wake huku ikichangia ukuaji wa mapato nchini kupitia makusanyo ya kodi mbalimbali," Vicky aliongeza.

# RC aagiza msako mkali wa matapeli waunganisha umeme

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuwasaka watu waliowatapeli wananchi fedha zao kwa madai kuwa wao ni wahandisi wa Tanesco, hivyo watawaunganishia umeme wa Rea majumbani.

Agizo hilo alilitoa jana katika kijiji cha Mnyaki wilayani Mpanda baada ya kupokea taarifa za malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa waliwapa watu fedha ili wawaunganishie umeme wa Rea lakini ni muda mrefu umepita bila kupata nishati hiyo.

Akiwa katika mkutano wa hadhara baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walimlalamikia kuwa kuna watu ambao walifika kijijini hapo na kuchukua fedha katika nyumba 181 wakidai kuwa wao ni watumishi wa Tanesco na watawaunganishia umeme wa Rea.

Mmoja wa wakazi hao John Nzigiwe alisema kuwa watu hao walikuwa wakichukua fedha hizo na kuahidi kufanya kazi hiyo ndani ya kipindi kifupi na kwa kuwa wananchi wanaisubiri nishati hiyo kwa hamu kubwa kwa muda mrefu waliwapa fedha.

"Sisi tuliamini kuwa ni wahusika, na tulikuwa tukitoa fedha na wao walikuwa wakituorodhesha majina, lakini mpaka sasa ni zaidi ya miezi mitatu hakuna kinachoendelea, tunashangaa hii maana yake nini?" Alihoji.

Hata hivyo kwa mujibu wa Mhandisi Anold Nzoli kutoka kampuni ya China Raiways Construction Electrification Bureau Group Co Ltd inayofanya kazi ya kusambaza umeme huo katika eneo hilo, kampuni hiyo haijafika eneo hilo na watu hao si watumishi wa kampuni hiyo.

Ndipo Homera alipoliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuwasaka watu hao ili wakamatwe na wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma hizo.




Meneja wa Kitengo cha Kuhudumia Wateja Wakubwa Airtel Tanzania, Alice Maziku, akimkabidhi kitanda cha upasuaji Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Mshanu Munde, mwishoni mwa wiki. Kampuni ya Airtel Tanzania kupitia mradi wa Airtel Tunakujali ilitoa kitanda cha upasuaji kwa kinamama wanaojifungua kwa Hospitali ya Mkurunga ikiwa ni juhudi za kusaidia jamii iiliyo kwenye mahitaji maalum. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEMC: Sabasaba fursa kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira, kutoa huduma za ulipaji wa tozo za tathmini ya athari kwa mazingira (EIA), ukaguzi wa mazingira (EA) pamoja na masuala mbalimbali yanayohusu mazingira.

NEMC imeshiriki katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa maarufu Sabasaba wakishiriki katika Banda la Katavi kwa madhumuni ya kuuhabarisha umma juu ya majukumu yake katika suala la mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika maonyesho hayo yanayoendelea jijini Dar es Salaam, Ofisa Mazingira Mwandamizi wa NEMC, Pendo Kundya, alisema kuwa dhumuni la NEMC kuwapo katika viwanja hivyo ni kutoa elimu ili kujenga uelewa mpana kwa wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji mazingira.

"Mudhumuni yetu ni kuendelea kuuhabarisha umma juu ya utunzaji wa mazingira na pia kuhamasisha juu ya katazo la serikali la matumizi ya mifuko ya plastiki na kutumia mifuko mbadala iliyothibishwa na mamlaka husika kutumiwa na jamii," alisema.

Aidha, Kundya aliongeza kuwa mazingira ni muhimu yakatunzwa ili athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira usituathiri kama nchini kwa kujijengea mazoea ya kufanya usafi katika mazingira yanayotuzunguka.

"Katika banda hilo NEMC wanatoa huduma mbalimbali ikiwemo kupokea tozo za EIA pamoja na EA kwa mwaka 2019//2020 kwa wadau ambao hawajalipa," Kundya alisema.

Alisema Baraza limesogeza huduma za malipo ya tozo za EIA na EA ili wadau wa mazingira waweze kuzilipia hapa kwani katika maonyesho haya wadau wengi hujitokeza ili kupata maelezo ya mambo mbalimbali yanayofanywa na kampuni au taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Mkaguzi wa Mazingira wa NEMC, Nelson Nyabise, alisema NEMC inaendelea kutoa elimu na mwongozo kwa wadau wa mazingira ambao hufanya shughuli za ukusanyaji, utunzaji na usafirishaji wa taka hatarishi kama betri chakavu, taka za kielektroniki na oil chafu ili zisiweze kuleta madhara kwa wananchi.

"Athari za taka hatarishi ni hatari kwa ustawi wa mazingira, hivyo katika banda letu tunaendelea kutoa elimu kuhusu namna nzuri ya kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha taka hatarishi ili zisilete madhara kwa wananchi," alisema Nyabise.

Naye Ofisa Mazingira wa NEMC, Elias Chundu, alipongeza mwitikio wa Watanzania katika kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusu mazingira huku wengine wakitoa maoni ambayo Baraza imeahidi kuyafanyia kazi.

"Kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa Watanzania katika kufuatilia masuala yanayohusu mazingira na hasa mkikumbuka hivi karibuni kulikuwa na marufuku ya utumiaji wa mifuko ya plastiki ambapo walitii marufuku hiyo pasipo kutumia nguvu," alisema Chundu.

Wananchi kadhaa waliotembelea banda hilo walitoa pongezi kwa baraza hilo katika kusimamia sheria na kanuni za mazingira na kutoa wito kuendelea kutoa elimu kupitia vyombo vya habari juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

"NEMC inafanya kazi nzuri kuhakikisha elimu ya utunzaji wa mazingira inawafikia mwananchi wote na nimefurahi kuwakuta katika maonyesho haya, hii inaonyesha ni namna gani wamejipanga katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya mazingira," alisema Mary Joshua alipotembelea banda la NEMC

Alisema zipo baadhi ya changamoto wanazotakiwa kuzifanyia kazi kama NEMC ikiwa ni pamoja na tatizo la kelele zinazotoka katika baa, kumbi za starehe na ibada za mikesha ambapo zinawaathiri wananchi wengi.

HABARI KIMATAIFA

## Unesco yautambua mji wa kale wa Iraq

**BAKU, Azerbaijan**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limeutambua mji wa kale wa Babylon kuwa eneo la kihistoria. Iraq imekuwa ikishinikiza tangu mwaka 1983 mji huo wa kale wa miaka 4,000 ujumuishwe katika orodha ya kifahari ya Umoja wa Mataifa.

Mji huo ulijulikana kwa bustani zake za kuning'inia, ambazo zilikuwa kati ya Maajabu Saba ya Dunia ya vitu vya kale duniani.

Miaka ya hivi karibuni eneo hilo limeharibiwa kufuatia ujenzi wa kasri la Saddam Hussein, na baadaye kutumiwa kama kambi ya kijeshi kwa vikosi vya Marekani.

Kamati ya Urithi wa Dunia ya Umoja wa Mataifa ilikutana nchini Azerbaijan kuamua kuhusu maeneo mapya ya kale ambayo yanastahili Kutambuliwa, ili yapewe tuzo kwa kuwa maeneo au nembo ya kihistoria inayozingatia umuhimu wa binadamu wote na kulindwa na mikataba ya kimataifa.

Ujumbe wa Iraq ulikaribisha hatua hiyo, ukisema kuwa huu ni utambuzi wa mchango wa Babylon katika ustaarabu wa Mesopotamia.

Haki miliki ya picha mfano wa lango la Ishtar, ambayo ilikuwa moja ya vitu asilia ambavyo ni sehemu ya vitu saba vya kushangaza duniani.

Ikitangaza uamuzi huo, Unesco ilisema: "Hatua hii inaashiria utambuzi wa ubunifu wa hali ya juu ya mji wa Babylon.

"Kuhusishwa kwa mji huo na moja ya maajabu saba ya vitu vya kale duniani. Pia ilionya kuwa maeneo hayo yako katika "hali mbaya" na kwamba yanahitaji kuhifadhiwa haraka iwezekanavyo.

**VOA**

# Serikali Botswana kukata rufani kupinga mapenzi ya jinsia moja

**GABORONE, Botswana**

SERIKALI ya Botswana itakata rufani dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu nchini uliohalalisha mapenzi ya jinsia moja, mkuu wa sheria amesema.

Mwezi Juni Mahakama Kuu ya Botswana iliondoa sheria ya kuwahukumu mashoga kutumikia kifungo hadi miaka saba uamuzi ambao ulisifiwa na taasisi za kimataifa pamoja na wanaharakati wanaowaunga mkono mashoga.

Serikali ya Botswana ilieleza kwamba itakata rufani dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu nchini humo ambao uliondoa sheria ya kuwahukumu mashoga na kukiuka sheria ambayo ilitoa adhabu kwa watu wa mapenzi ya jinsia moja kwenda jela hadi miaka saba.

Uamuzi huo wa mahakama ulitolewa mwezi Juni mwaka huu ambao ulisifiwa na taasisi za kimataifa pamoja na wanaharakati wanaotetea haki za mashoga uliomaanisha kwamba Botswana ni moja ya nchi za Kiafrika ambayo inaidhinisha mahusiano ya jinsia moja.

Mwanasheria Mkuu nchini Botswana, Abraham Keetshabe, alieleza katika taarifa iliyotolewa Ijumaa jioni kwamba Mahakama Kuu ilikosea kutoa uamuzi wake na kurudi kwenye sheria za enzi ya ukoloni.


"Nimesoma kwa kina uamuzi huo wa kurasa 132 na maoni yangu ni kwamba Mahakama Kuu ilifanya makosa katika kufikia uamuzi huu," Keetshabe amesema katika taarifa iliyotolewa jana Ijumaa.

Uamzi huo ulipongezwa na wengi na kutajwa kuwa ni kupiga hatua katika kuimarisha haki za wapenzi wa jinsia moja Afrika.

Lakini mkuu wa sheria nchini humo Abraham Keetshabe amesema majaji katika mahakama hiyo wamefanya makosa.

Ameongeza kwamba ataipeleka kesi hiyo katika mahakama ya rufani, lakini hakutoa ufafanuzi zaidi kwa misingi ya rufani hiyo.

**VOA**



Mjumbe wa Umoja wa Afrika, Sudan, Mohamed al-Hacen Lebatt (kushoto), akiwa na Naibu Mkuu wa Baraza la Utawala wa Jeshi, Jenerali Mohamed Hamdan Dagalo, katika mkutano wa waandishi wa habari mjini Khartoum, Sudan. **PICHA: VOA**

# Afichua siri kaburi la filauni chini ya piramidi

**CAIRO, Misri**

MWANAAIKOLOJIA wa kupiga mbizi ameieleza BBC kuhusu jitihada aliyopitia kulifikia kaburi la firauni chini ya piramidi. Pearce Paul Creasman na kikosi chake ni watu wa kwanza kuingia katika kaburi hilo katika kipindi cha miaka 100 na katika muda huo, imekuwa vigumu kulifikia kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha maji baharini.

Creasman ameiambia BBC kwamba ni mara ya kwanza uchimbaji wa chini ya maji unafanyika katika akiolojia nchini Sudan, eneo la jadi alikozikwa Nuri na aligundua vitu vilivyotengenezwa kwa udongo na dhahabu iliyopondwa.

"Dhahabu hiyo ilikuwa ingalipo - sanamu hawa wadogo wa vigae walikuwa wamefunikwa kwa dhahabu. Na wakati maji yaliiharibu vigae vilivyokuwa chini, chembe chembe za dhahabu bado zilikuwapo," ameeleza.

Anaamini zawadi hizo zilikuwa ni za Nastasen, firauni mdogo alioyetawala ufalme wa Kush tangu 335 BC hadi 315 BC.

Dhahabu hii huenda ingelichukuliwa na wezi lau kama hakunge kuwapo na kiwango kikubwa cha maji yanayozuia kufikiwa kaburi hilo, mwanaakiolojia wa chini ya maji Kristin Romey ameandika katika National Geographic.

Creasman ameiambia BBC kwamba kikosi hicho "kilichimba chini kadri ya uwezo wao" chini ya ngazi yenye vidaraja 65 iliolekea katika mlango wa liliko kaburi hilo lakini "tulishuka hadi katika daraja la 40 mpaka tulipofika chini sakafuni na tukatambua hatuwezi kushuka tena pasi kuzamisha vichwa".

Walitumia bomba iliyotoa hewa ya oxygen kutoka juu ardhini wakati walipopiga mbizi mwezi Januari na kueleza kwamba walistaajabishwa kwa walichokigundua:

"Kuna sehemu tatu, zilizo na sehemu ya juu iliyo chongwa zenye ukubwa wa basi dogo la usafiri unaingia katika sehemu moja na kutokea katika nyingine ni giza, unajua uko ndani ya kaburi, iwapo hukuwasha tochi," alisema.

***BBC.***

# Marekani yakaribisha mkataba kumaliza mgogoro wa Sudan

**WASHINGTON, Marekani**

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Marekani imetoa wito wa kukuza kile inachokiita baraza la uhuru lenye mzunguko wa madaraka kwa nafasi ya rais kutoka upande wa jeshi na kiraia kwa miaka mitatu.

Marekani inasema inaukaribisha mkataba wa kushirikiana madaraka uliobuniwa kumaliza miezi kadhaa ya ghasia za kisiasa nchini Sudan.

Mkataba huo uliafikiwa Ijumaa kati ya viongozi wanaoandaa maandamano na majenerali wanaotawala nchi baada ya kufanyika mazungumzo ya siku mbili. Marekani imetoa wito wa kukuza kile inachokiita baraza la uhuru lenye mzunguko wa nafasi ya rais kutoka upande wa jeshi na kiraia kwa miaka mitatu.

Wizara ya Mambo ya Nje Marekani ilisema hii ni hatua muhimu kusonga mbele. Ilielezea matumaini kwamba mkataba utaongoza kuundwa kwa serikali ya muda inayoongozwa kiraia ambayo ndio inasisitizwa na watu wa Sudan. Nchi ya Sudan imeingia kwenye matatizo ya kisiasa tangu majenerali walipomwondoa Rais wa muda mrefu Omar Al-Bashir kwa njia ya mapinduzi mwezi Aprili kufuatia miezi kadhaa ya maandamano ya umma nchi nzima.

***VOA***

# HABARI PICHANI



Mwalimu wa Veta Singida, Cleophas Mkungu, akitoa maelezo kwa wananchi kuhusu mashine ya kufulia nguo inayoendeshwa kwa mikono katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA:MIRAJI MSALA**



Daktari wa Mifugo kutoka Kampuni ya Salibab Pellet Co. Ltd (Hill Feeds), Christopher Kileo (kushoto), akitoa maelezo kwa wananchi kuhusu chakula cha mifugo katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mratibu wa Gesi Asilia kutoka Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), Dk. Esebi Nyari, akitoa maelezo kwa wananchi kuhusu gari inatumia gesi katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana**. PICHA: MIRAJI MSALA**



Wananchi wakiwa kwenye mizunguko ya kutembelea mabanda katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wananchi wakiwa wamepumzika baada ya mizunguko katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Kaimu Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji Brela, Frederick Mahawi (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi waliotembelea kuijua Brela katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA:MIRAJI MSALA**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

## NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI,** Wanahitajika IT – Diploma, Sales Lady, Messenger – awe mvulana. Elimu kidato cha nne/ cha sita. Wawe wazoefu wa kutosha. Mawasiliano: 0715 885533. Email: jmtofficetraders96@gmail.com au jmtofficetraders@gmail.com.

## MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Haji Ramadhani Isihaka** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T762 BBA** gari aina ya **TOYOTA CHASER,** yenye chasis namba **GX1000078387.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **TAN/RB/250/2019**

115312302


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa

Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MILAN YATHIBITISHA KUMSAJILI HERNANDEZ

**MILAN, Italia**

KLABU ya AC Milan imethibitisha kuwa imemsajili beki wa pembeni, Theo Hernández kwa mkataba wa miaka mitano kutoka Real Madrid.


Beki huyo mwenye umri wa miaka 21 alihamia pale kwenye dimba la Santiago Bernabéu kwa euro milioni 24 kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja, Atletico Madrid mwaka 2017, lakini alilazimika kupelekwa kwa mkopo Real Sociedad baada ya kushindwa kupata namba kwa Los Blancos.

Huku Rais wa Real Madrid, Florentino Pérez kwa sasa akiwa anataka kupata fedha za kusajili wachezaji wapya, huku tayari akiwa ametumia euro milioni 300, Milan imethibitisha kwenye tovuti yake kumsajili nyota huyo.

Taarifa ya Milan ilisomeka: "AC Milan inatangaza kufikia makubaliano na Real Madrid kumsajili Theo Bernard Fran ois Hernández (Theo Hernández).

"Beki wa kushoto wa Ufaransa amejiunga na klabu yetu kwa mkataba wa kudumu wa miaka mitano hadi Juni 30 mwaka 2024."

Nayo Real Madrid ilithibitisha kwenye tovuti yake kwa taarifa iliyosomeka: "Real Madrid CF na AC Milan imekubaliana juu ya uhamisho wa Theo Hernández."



# KOCHA MISRI ATIMULIWA, RAIS WA 'TFF' YAO AJIUZULU

**CAIRO, Misri**

KOCHA wa Timu ya Soka ya Taifa ya Misri, Javier Aguirre, ametimuliwa baada ya 'Mafarao' kutolewa kwenye michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) kwa kufungwa bao 1-0 na Afrika Kusini.

Taarifa ya Shirikisho la Soka la Misri (EFA), iliyowekwa kwenye tovuti yao jana ilisema kwamba, kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, amefukuzwa baada ya timu yao kutolewa kwenye fainali hizo za Afcon ambazo zinaendelea nchini humo.

Baada ya mchezo wa juzi jijini Cairo, kocha huyo raia wa Mexico alisema anastahili lawama kwa kuondolewa kwenye michuano hiyo na kwamba, jana angejadiliana na EFA kuhusu hatima yake.

Muda mfupi baada ya kocha huyo kutimuliwa, Rais wa EFA, Hany Abou-Rida naye alitangaza kujiuzulu na akawataka wasaidizi wake waandike barua za kuachia ngazi.

Aguirre alianza kuifundisha timu hiyo Agosti mwaka jana, na tangu wakati huo Mafarao hao wamecheza mechi 12, wameshinda tisa, wametoka sare moja, huku wakifungwa mechi mbili, ikiwamo ya juzi usiku.

# Loftus-Cheek atia saini mkataba mpya

**LONDON, England**

KIUNGO wa Chelsea, Ruben Loftus-Cheek ametia saini mkataba mpya wa miaka mitano pale Stamford Bridge, utakaomweka klabuni hapo hadi mwaka 2024.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 amejiimarisha yeye mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza kwa miamba hao wa London Kaskazini.

Ingawa Chelsea haitafanya usajili wa wachezaji wapya kipindi hiki baada ya kufungiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa, Fifa, Mateo Kovacic ametia saini mkataba wa kudumu na sasa klabu imethibitisha Loftus-Cheek amesaini mkataba wa miaka mitano.

Chelsea hivi karibuni ilimtangaza mchezaji wake wa zamani, Frank Lampard kuwa kocha wao mpya.




"Nina furaha kubwa kuendelea kuwa hapa na kusaini mkataba mpya wa miaka mitano. Ni sehemu ambayo nimekuwa nikicheza hapa, na sasa nina uhakika nitacheza hapa kwa muda mrefu zaidi," alinukuliwa Loftus-Cheek na tovuti ya Klabu ya Chelsea.

"Kwa sasa nitaendelea kucheza hapa kwa muda wa miaka mitano mingine, ni wakati mzuri kwangu kuendelea kuwa kwenye klabu ambayo imekuwa ndoto yangu, ni ya uhakika wa kuwa na wakati bora zaidi.

"Pamoja na yote, naishukuru klabu kwa kuniamini na kuniongeza mkataba mpya, kwani imeonyesha kwamba bado mimi ni mchezaji wa thamani katika klabu hii," alisema.



# MESSI AWALALAMIKIA WAAMUZI KWA UPENDELEO COPA AMERICA

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, hakumaliza mchezo wa kutafuta mshindi wa tatu kwenye michuano ya Copa America, usiku wa jana dhidi ya Chile, baada ya kutolewa kwa kadi nyekundu.

Mwamuzi wa mchezo huo, Mario Diaz de Vivar aliwatoa Messi na Gary Medel baada ya kukwaruzana uwanjani.

Kitendo hicho hakikumfurahisha Messi na aliwaambia waandishi wa habari kuwa ulikuwa ni mwendelezo wa mipango mibovu na upendeleo unaofanywa na Shirikisho la Soka la Amerika Kusini, CONMEBOL.

Mchezo ulimalizika kwa Argentina kupata ushindi wa mabao 2-1, mabao yakifungwa na Paulo Dyabala na Sergio Aguero, huku bao pekee la Chile likifungwa na Arturo Vidal, lakini Messi hakuonekana wakati wa kupewa zawadi baada ya mchezo kumalizika.

"Hakuna shaka yoyote, mazingira yote haya yanatengenezwa kwa ajili ya kuwafaidisha Brazil na ninaamini VAR na hata waamuzi hawatokuwa sehemu ya maamuzi sahihi katika mchezo wa fainali," alisema Messi.

"Sitaki kuwa mmoja wa wahusika katika rushwa ya aina hii, hatukutakiwa kuwa katika uonevu huu ambao tumekutana nao katika Copa America ya mwaka huu.

"Tulipaswa tufike mbali katika mashindano lakini tulizuiwa tusifike fainali, rushwa, waamuzi na vingine vingi vimewanyima watu uhondo wa kushuhudia kandanda safi."

"Mimi mara zote nasema ukweli na ni muwazi, ndicho kinachonifanya kuwa mtulivu hivi," aliongeza Messi.

Michuano hiyo ilimalizika jana Jumapili kwa fainali kupigwa kati ya wenyeji Brazil na Peru.

# Chelsea yathibitisha kumuuza Morata



**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imethibitisha kwamba, imemuuza mshambuliaji wao, Alvaro Morata kwa Atletico Madrid.

Morata atabakia anacheza kwa mkopo Atletico kwa msimu wa 2019-20 kama klabu hizo zilivyokubaliana Januari, kabla ya kusajiliwa moja kwa moja Julai Mosi mwaka 2020 kwa ada inayotajwa kuwa ni pauni milioni 58.

Taarifa kutoka tovuti ya Klabu hiyo ya Chelsea ilisomeka: "Chelsea na Atletico Madrid wamefikia makubaliano ya uhamisho wa kudumu wa Alvaro Morata.

"Tungependa kumshukuru Alvaro kwa mchango wake na tunamtakia kila la heri katika maisha yake ya soka."

Morata aliweka rekodi ya usajili kwa Chelsea wakati aliponunuliwa kutoka Real Madrid kwa ada ya pauni milioni 60.

Alianza vizuri katika maisha yake ya soka nchini England, akifunga mabao manane katika mechi zake saba za mwanzo kwenye mashindano yote.

Lakini baadaye kiwango chake kinashuka huku akikabiliwa na majeruhi na alipoteza namba mbele ya Olivier Giroud.

Ujio wa Maurizio Sarri pale Chelsea kuchukua nafasi ya Antonio Conte kipindi cha majira ya joto kilichopita kulifufua matumaini ya Morata, lakini akajikuta kwenye wakati mgumu na Chelsea walimpeleka kwa mkopo Atletico Januari, huku Gonzalo Higuain akichukua nafasi yake kutoka Juventus.

# UNITED KUTOMWONGEZA MSHAHARA DE GEA

**MANCHESTER, England**


KLABU ya Manchester United imesema kwamba, haitamwongeza mshahara golikipa wake, David De Gea ambaye anahusishwa na mpango wa kutaka kuondoka klabuni hapo.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, taarifa kutoka kwenye timu hiyo zinasema mabosi wa De Gea wamevunja ukimya na kwa kusimamia misimamo yao ambapo wamenukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari kuwa wapo tayari kumpa mshahara wa pauni 350,000 na si vinginevyo.

Mabosi hao wa United wamemwambia kipa huyo kwamba hawatomwongeza fedha zaidi ya hapo ambayo watakua wakimlipa kwa wiki.

Mmoja wa maofisa wa United amekaririwa akisema kwamba, uwezekano wa kumpa mshahara mkubwa zaidi De Gea haupo kwa sasa.

"Vyombo vingi vinaandika kwamba tutamwongeza mshahara anaoutaka De Gea, lakini ukweli ni kwamba hakuna mpango kama huo," alinukuliwa ofisa huyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ATAMANI KUREJEA BARCELONA

●●●Lakini inaelezwa kuwa mabosi wake wa PSG hawataki kumuuza mshambuliaji huyo...

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amesema anajua kuwa Neymar anataka kuondoka Paris Saint-Germain, ingawa mabingwa hao wa Ufaransa hawataki kumuuza.

Bartomeu pia alithibitisha kwamba, wameanza mazungumzo na Atletico Madrid juu ya kumsajili mshambuliaji, Antoine Griezmann.

Kwa mujibu wa ESPN FC mapema wiki hii Barca ilisema kwamba haijaondoa uwezekano wa kumsajili mshambuliaji huyo wa Ufaransa na kuna uwezekano wa kumchukua Neymar, ambaye aliondoka kwa miamba hao wa Katalunya kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222.

Barca wanaamini kwamba dili la usajili wa mchezaji huyo linaweza kufanikisha na ESPN FC imebainisha kuwa Philippe Coutinho anaweza kutumika kama chambo kwa kupelekwa kule PSG.

"Tunajua kwamba, Neymar anataka kutoka PSG, lakini PSG hawataki kumuuza, hivyo hakuna kesi kwa Neymar," alisema Bartomeu wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari Ijumaa.

Alipoulizwa kama ni jambo zuri kwake kutaka kumsajili tena Neymar, rais huyo alijibu: "Hatuwazungumzii wachezaji kutoka kwenye timu nyingine."

Awali iliripotiwa kwamba, nahodha wa Barca, Lionel Messi alikutana na Bartomeu kwa ajili ya mazungumzo ya kuhakiisha Neymar anarudi katika dimba hilo la Camp Nou.

"Ngoja tumalize uvumi huu," alisema Bartomeu alipoulizwa kama ni kweli alikutana na Messi kujadili suala hilo.

"Messi hawezi kuiambia Barcelona mchezaji gani wa kumsajili. Yeye huwa anataka tu tuwe na timu yenye ushindani."

Bartomeu pia alifunga mlango juu ya uvumi wa kuondoka kwa Ousmane Dembele klabuni hapo akisema kwamba, winga huyo wa Ufaransa ni mchezaji muhimu zaidi kwenye kikosi hicho.

"Dembele ni mchezaji kijana, mwenye kipaji ambaye anaongeza kitu tofauti kwa timu," alisema.

"Kumwangalia akicheza uwanjani ni jambo la kuvutia zaidi na mara zote anakuwa tofauti, hivyo kwa upande wangu yeye ni bora zaidi kuliko Neymar."

Na pia Bartomeu alielezea kwamba Barca kwa sasa wamefungua majadiliano na Atletico kwa ajili ya kumsajili Griezmann. Kulikuwa na kikao Alhamisi kati ya maofisa watendaji wa klabu hizo mbili, Oscar Grau na Miguel Angel.

## KWA UFUPI

**COSTA ATAKIWA EVERTON**

MMLIKI wa Everton, Farhad Moshiri anataka klabu hiyo maarufu kwa jina la The Toffees kuhakikisha inapata saini ya straika wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Diego Costa (30), ambaye anatarajia kutoa tamko kuhusu usajili wake katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail on Sunday)***

**POGBA MAFICHONI**

MABOSI wa Manchester United wamesema kuwa hawana uhakika kama kiungo wao, Paul Pogba (26) atajiunga na kikosi cha timu hiyo kinachotarajia kwenda kuweka kambi nchini Australia ili kujiandaa na msimu mpya, kwa sababu hakifahamu mahali alipo Mfaransa huyo. (Sunday Mirror)

**FERNANDINHO SAFI**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anajiandaa kumpa mkataba mpya kiungo, Fernandinho (34) ikiwa ni siku chache tangu mabingwa hao wa Ligi Kuu England walipomsajili kwa dau lililoweka rekodi nyota, Rodri ili kurithi mikoba ya Mbrazil huyo. ***(Sun on Sunday)***

**DE GEA KIMEELEWEKA**

KIPA David de Gea anajiandaa kufanya uamuzi kuhusu hatima yake katika kikosi cha Manchester United kwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitano ambao atalipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki ndani ya klabu hiyo ya Old Trafford. ***(Sunday Mirror)***

**LEICESTER YAIBANIA UTD**

MANCHESTER United imetajwa kuwa ndio klabu pekee ambayo imeonyesha kuhitaji saini ya beki wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, lakini klabu hiyo maarufu Foxes imeweka wazi kwamba inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 85 ili kumuuza mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Sun on Sunday)***

**FRASER ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL imeweka wazi kwamba inamhitaji winga wa Bournemouth ambaye ni raia wa Scotland, Ryan Fraser (25), ili kuchukua nafasi ya nyota wa Crystal Palace, Wilfried Zaha. ***(Sunday Mirror)***

**NEUER KUONDOKA BAYERN**

WAKALA wa golikipa, Manuel Neuer ambaye ana umri wa miaka 33, amesema kuwa Mjerumani huyo anajiandaa kuondoka Bayern Munich katika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Suddeutsche Zeitung - in German)***

**ROSE MAMBO MAGUMU**

BEKI wa Timu ya Taifa ya England, Danny Rose (29), anaongoza katika orodha ya wachezaji nane ambao wamekalia kuti kavu katika kikosi cha Tottenham ambacho kinajiandaa kujiimarisha katika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Mail on Sunday)***

**SERGEJ AKARIBIA UTD**

WAKALA wa kiungo wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic amesafiri kuelekea London kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Manchester United ili kujadili uhamisho wa Mserbia huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Sport Mediaset - in Italian)***

**AYEW KUTUA PALACE**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ghana, Jordan Ayew (27) atajiunga na Crystal Palace akitokea Swansea kwa ada ya pauni milioni 2.5 mara baada ya kumalizika kwa Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), ambazo zinaendelea nchini Misri. ***(Guardian)***

**LUKAKU- NATAKA KUONDOKA**

STRAIKA wa Manchester United, Mbelgiji Romelu Lukaku, amesema anataka kuondoka katika klabu hiyo na tayari ameanza kupata ofa kutoka Juventus na Napoli, zote za Italia. ***(Sun on Sunday)***

**LIVERPOOL, BARCA VITANI**

BEKI wa kushoto wa Real Betis na Timu ya Taifa ya vijana ya Hispania ya umri chini ya miaka 21 (U-21), Junior Firpo amezivutia klabu za Liverpool na Barcelona. ***(Muchodeporte - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

# YANGA YATUA MORO KUZINOA SILAHA ZAKE

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Yanga cha jijini Dar es Salaam kimetua mkoani Morogoro tayari kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine itakayoshiriki, imeelezwa.

Mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga pia itashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la FA na michuano ya Kombe la SportPesa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, alisema wameamua kwenda kuweka kambi Morogoro kwa sababu wanaamini wachezaji watapata utulivu na nafasi nzuri ya kutekeleza programu zote zinazotakiwa na benchi la ufundi.

Msolla alisema kuwa wachezaji wote waliosajiliwa wataanza mazoezi ya timu hiyo leo na hii itasaidia kuwafanya wawe tayari kushindana, mara ligi itakapoanza.

"Kesho (leo) asubuhi timu yetu itasafiri kuelekea Morogoro ili kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu," alisema Msolla.

Kiongozi huyo alisema anamini Yanga itakuwa na kikosi chenye ushindani katika msimu ujao kutokana na usajili mzuri wa wachezaji walioufanya.

"Lengo letu ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu ujao, kikubwa mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano ili tutimize malengo yetu," alisema kocha huyo wa zamani wa Reli, Mirambo na Taifa Stars.

Alisema kwamba amefurahishwa na hali ya nidhamu iliyoonyeshwa na wachezaji wao baada ya jana kutakiwa kuwasili klabuni, na kueleza kwamba huo ni mwanzo wa kuwa na msimu wenye mafanikio.

"Nimefurahi kuona nidhamu imeanza, asilimia 95 ya wachezaji wamejitahidi kuripoti kambini, nidhamu waliyoionyesha imenifurahisha, wameonyesha kutii amri ya uongozi wao," Msolla alisema.

Yanga ilimaliza msimu uliopita katika nafasi ya pili, nyuma ya mabingwa Simba wakati Azam FC ilishika nafasi ya tatu huku KMC FC wao walimaliza katika nafasi nne.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde (kulia), akimkabidhi zawadi mshindi wa pili wa mbio za Dodoma City Marathon, Fred Kwezi, kutoka Kenya baada ya kufanya vema katika mbio hizo zilizofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Makocha Zanzibar watakiwa kushirikiana

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Chama cha Soka Wilaya ya Unguja Mjini, Hassan Haji Hamza, amewataka makocha wa Zanzibar kuwa na ushirikiano ili kujenga mustakabali imara wa kuendeleza soka la visiwani hapa.

Hamza alisema hayo jana katika ufunguzi wa mafunzo ya siku sita ya makocha wa makipa yaliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) ambayo yalifanyika kwenye Uwanja wa Amaan.

Kiongozi huyo alisema kumekuwa na tabia ya makocha wa soka kutokuwa na ushirikiano katika kazi zao, jambo ambalo linaufanya mpira wa Zanzibar kuporomoka na kuwasisitiza kubadili tabia zao kwa faida ya mchezo huo.

"Nimefanya utafiti na kubaini kitu kimoja kibaya ambacho kinaturudisha nyuma ni kwamba walimu wa soka Zanzibar wana roho mbaya, maisha amepanga Mungu, hata ufanye nini huwezi kumshusha mwenzako, ni vema mkashirikiana na kupendana ili kurahisisha kazi yenu," alisema Hamza.

Aliongeza kuwa wapo baadhi ya makocha wenye uelewa mdogo lakini kwa makusudi wanashindwa kuwafuata wale ambao wana uwezo wa juu kwa ajili ya kujifunza, kutokana na kutokuwa na ushirikiano baina yao.

"Kutopendana na kushirikiana kunapelekea kuharibu kwa makusudi na sio jambo jema katika mpango wa maendeleo ya soka la Zanzibar, husuasani katika kuwajenga makipa na wachezaji wengine wenye vipaji ambao wanapatikana visiwani Zanzibar, tubadilike," Hamza aliongeza.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo, Abdillahi Silima, aliiomba ZFF kuhakikisha inasimamia kikamilifu kanuni yake ya klabu zote kutumia makocha wenye vyeti vinavyotambulika ramsi ili kuwapa nafasi walimu waliojiendeleza kutumia elimu waliyoipata kuwanoa wachezaji wa Zanzibar.

Silima aliiomba pia ZFF kutoa vitambulisho maalumu vya kuingilia uwanjani ili kuepusha usumbufu wakati wa kwenda kutazama mechi mbalimbali zinazochezwa visiwani hapa.

Naye Mkufunzi wa mafunzo hayo, Saleh Ahmed Machupa, alisema kuwa amefarijika kuona mahudhurio katika mafunzo hayo yamekuwa makubwa na vile vile washiriki wote kufaulu kozi hiyo waliyokuwa wanaifanya.

## Mbabe atamba kumpiga Kamata

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Shabani maarufu Dulla Mbabe, ametamba kuibuka na ushindi dhidi ya mpinzani wake, Paul Kamata katika pambano la raundi 10 litakalofanyika Julai 27 mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dulla Mbabe, alisema amejiandaa vizuri kuhakikisha siku ya pambano hilo anawafurahisha mashabiki wake.

"Nimejipanga vizuri kwa ajili ya pambano langu ambalo nitapanda ulingoni siku chache zijazo, ninaahidi mashabiki wangu watapata furaha, nitafanya vizuri, wasiwe na wasiwasi," alisema bondia huyo.

Aliongeza kuwa anaamini mafunzo anayopata chini ya kocha wake, Pelege Damme, yanampa nguvu na kumweka tayari kuchukua mkanda wa pambano hilo.

"Nashukuru bondia wangu anaendelea vizuri na morali yake ipo juu, ninafanya kila kinachotakiwa kuhakikisha anafanya vizuri, lengo letu ni kupata ushindi katika pambano hilo, najua siku zilizobakia ni chache," alisema Pelege.

## Makocha wapya riadha wanolewa

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

SHIRIKISHO la Riadha Tanzania (RT) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wameendesha kozi ya ukufunzi wa mchezo huo ya ngazi ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu wa Pili wa RT na Mkufunzi wa kozi hiyo, anayetambuliwa na Shirikisho la Mchezo huo duniani (IAAF), Dk. Hamad Ndee, alisema kozi imefanyika kwa mafanikio na imeshirikisha washiriki 25.

Dk. Ndee alisema kuwa IAAF iliamua kubadili mfumo wake wa ngazi za ualimu wa riadha kutoka nne hadi tatu na kwa kuunganisha ngazi ya kwanza na ya pili.

"Mpango wa RT wa muda mrefu ni kuendesha mafunzo ya ngazi ya kwanza na hatimaye ngazi zote nchini, RT itashirikiana na mikoa yote kwa kadri iwezekanavyo ili kuendesha mafunzo haya kwa sababu inaamini hapa ndipo mahali muhimu katika kuandaa wachezaji, lakini kwanza tumeanza kwa kushirikiana na Idara ya Elimu kwa Michezo na Sayansi ya Michezo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa wanafunzi wanaotaka kuwa makocha wa mchezo wa riadha," alisema Dk. Ndee.

Naye Said Mohamed Abdulla, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo alisema kuwa alivutiwa kuhudhuria kozi hiyo kwa lengo la kuongeza ujuzi zaidi katika sekta ya michezo na anaahidi kuitumia kwa vitendo elimu hiyo aliyoipata.

# Michezo

Jumatatu Julai 8, 2019

Nipashe





Neymar atamani kurejea Barcelona

HABARI UK 30



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kulia), akitoa ufafanuzi baada ya kumaliza kikao chake na Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, kilichofanyika juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# STARS, AMUNIKE WAACHANA RASMI

Ni baada ya kupata matokeo mabaya Afcon, mrithi wake aanza kusakwa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akisema kuwa na imani kubwa na Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, taarifa za ndani zinaeleza kwamba kibarua cha kocha huyo kuifundisha timu hiyo kimefikia tamati.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zinasema kuwa tayari Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Mnigeria huyo wamefikia makubaliano ya kuvunja mkataba.

Taarifa zaidi zinasema kuwa TFF ambayo iko chini ya Rais, Wallace Karia, imeshaanza mchakato wa kusaka mrithi wa Amunike, ambaye ataiongoza Taifa Stars katika mchezo wake wa kwanza wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) dhidi ya Kenya, utakaochezwa baadaye mwezi huu.

Licha ya kuwa ndiye kocha aliyefanikiwa kuipeleka Taifa Stars katika fainali za Afcon baada ya miaka 39, Amunike alionekana kuivuruga TFF katika mambo mbalimbali, akianzia kwenye uteuzi wa wachezaji.

Nipashe lilifahamu mapema kuwa Amunike amekalia kuti kavu, tangu baada ya Taifa Stars kupoteza mechi ya pili ya Kundi C dhidi ya Kenya maarufu, Harambee Stars, baada ya kiongozi mmoja wa juu wa shirikisho hilo kusema kwamba, amekasirishwa na namna kikosi chao kilivyokuwa kikicheza kwenye fainali hizo.

Pia alisema alikasirishwa na kauli ya Mnigeria huyo kwamba Taifa Stars haikuwa tayari kushindana kwenye fainali hizo, wakati siku moja kabla ya kucheza na majirani zao hao, mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona alisema anaamini atapata matokeo mazuri katika mechi hiyo kwa sababu wanakutana na timu ambayo wachezaji wake wanajuana na kuzungumza lugha moja.

Rais wa TFF, Wallace Karia na katibu wake, Wilfred Kidao, wote hawakupatikana jana kuelezea uvumi huo, huku pia baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya shirikisho hilo wakiwa hawafahamu lolote.

Mapema jana, Waziri Mwakyembe ambaye alikutana na Amunike, alisema kuwa kinachohitajika ni suala la muda tu, kwani Mnigeria huyo amemweleza mipango mikubwa ya kiufundi aliyonayo kwa Taifa Stars ili iweze kufanya vizuri katika mashindano yajayo. Mwakyembe amesema kwamba Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika 2019 zinazoendelea nchini Misri zimebeba uzito wa kipekee kwa nchi ya Tanzania baada ya kukaa nje kwa miaka 39 na kufuzu kushiriki katika mashindano hayo licha ya kufungwa mechi zote tatu za Kundi C dhidi ya Senegal, Algeria na Kenya.

"Mimi nimefurahi sana kukaa na mwalimu, na yeye pia amefurahi kukaa na serikali, ili tujuwe mwenzetu maoni yake ni nini kuhusu timu ya Taifa, tufanyaje kujipanga ili kesho kutwa turejee tena Afcon, lakini safari hii tukirejea kila mtu awe na wasiwasi kuwa hii sio timu nzuri kukutana nayo," alisema Mwakyembe.

Alieleza namna Uganda walivyojipanga baada ya kutoka katika fainali za mwaka 2015, ambapo mwaka huu walirejea wakiwa imara na kuonyesha ushindani katika mechi zake zote walizocheza.

Mwakyembe amesema kuwa Amunike amependekeza mazoezi zaidi kwa wachezaji wa Stara kwa kucheza mechi za kirafiki kimataifa angalau mara tatu kwa mwaka ili kuwapa wachezaji uzoefu wa mashindano ya kimataifa.

# Samatta: Ndoto zangu zitatimia

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa Tottenham Hotspurs na Harambee Stars ya Kenya, Victor Wanyama, amemkaribisha rasmi nahodha wa Taifa Stars na mshambuliaji wa KRC Genk, Mbwana Samatta katika Ligi Kuu England msimu ujao.

Samatta ambaye bado ana mkataba na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji, ameweka wazi kwamba anahitaji kwenda kukutana na changamoto mpya.

Tayari klabu mbalimbali za England zimeonyesha nia ya kumhitaji mshambuliaji huyo wa zamani wa Simba ni pamoja na Leicester City, Middlesbrough na Aston Villa huku dau lake likitajwa kuwa ni sawa na Sh. bilioni 34 za Tanzania.

**"Ilikuwa ni nafasi nzuri kucheza na mmoja wa wachezaji bora na wa mfano wa kuigwa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, tunajivunia uwepo wako ndani ya Afrika Mashariki," alisema Samatta.**

Naye Wanyama alijibu kuwa: "Nashukuru sana kaka yangu, na ni matarajio yangu kukuona katika Ligi Kuu England msimu ujao, tuendelee kupeperusha bendera ya Afrika Mashariki."

Samatta na Wanyama walikutana katika Kundi C kwenye Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), ambazo bado zinaendelea nchini Misri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >